

# Ushuhuda wa Mababu zetu wa Kiroho Kuhusiana na Uungu

Umekusanywa na
Deyan Delchev

# Yaliyomo

Utangulizi ........ 5
Ushuhuda wa Waanzilishi wa Uadventista ........ 8
Joseph Bates ........ 13
Roswell Fenner Cottrell ........ 15
Joseph Birchard Frisbie ........ 18
Joseph Harvey Waggoner ........ 19
James Springer White ........ 22
Merritt E. Cornell ........ 26
John Nevins Andrews ........ 27
John Norton Loughborough ........ 29
Uriah Smith ........ 31
Stephen Nelson Haskell ........ 34
George Ide Butler ........ 35
John Gottlieb Matteson ........ 35
Sarepta Myrenda (Irish) Henry ........ 36
Dudley Marvin Canright ........ 36
Alonzo Trevier Jones ........ 38
Hampton Watson Cottrell ........ 39
James Edson White ........ 39
William Clarence White ........ 39
Milton Charles Wilcox ........ 40
Ellet J. Waggoner ........ 42
William Warren Prescott ........ 46
Judson Sylvaneous Washburn ........ 46
Charles S. Longacre ........ 49
WAANZILISHI WENGINE ........ 55
C. W. Stone ........ 55
A. J. Dennis ........ 55
A. J. Morton ........ 56
D. W. Hull ........ 56
J. M. Stephenson ........ 56

# Utangulizi

**Review and Herald**

**Kazi ya Wakati Huu**

***25 Mai 1905***

*Aya 21-28*

## Majarida Yetu

Mungu amenipa nuru kuhusiana na majarida yetu. Nuru hii ni nini? — Amesema kwamba waliokufa watazungumza. Kwa njia gani? — kazi yao itawafuata. Tunapswa kurudia maneno ya waanzilishi katika kazi yetu, ambao walijua gharama ya kutafuta ukweli kama hazina iliyositirika, na ambao walitenda kazi **ili kuweka msingi wa kazi yetu**. Walisonga mbele hatua kwa hatua chini ya athari ya Roho wa Mungu. Mmoja baada ya mwingine waanzilishi hawa wanatoweka. Neno ambalo nilipewa ni, wacha kile ambacho watu hawa waliandika kitambo kitolewe upya. Na katika "*The Signs of the Times*" wacha makala yasiwe marefu au toleo lisiwe laini. Usijaribu kubana kila kitu katika ukurasa mmoja. Wacha toleo liwe nzuri, na wacha bidii ya uzoefu unaodumu uandikwe kwenye karatasi.

Sio kitambo sana nilichukua nakala ya Mwangwi wa Bibilia. Nilipo iangalia kwa ndani, niliona makala ya Mzee Haskell na mengine ya Mzee Corliss. Nilipoweka karatasi hii chini, nilisema, makala haya lazima yachapishwe tena. Kuna ukweli na nguvu ndani yake. Watu walinena walivyoongozwa na Roho Mtakatifu.

**Wacha ukweli ambao ni msingi wa imani yetu utunzwe mbele ya watu wetu. Wengine wataondoka kwenye imani, wakizisikiliza roho zidanganyazo na mafundisho ya mashetani.** Wanazungumza kuhusu sayansi; lakini sio sayansi ya wokovu. Sio sayansi ya unyenyekevu, ya kuwa wakfu, au ya utakaso wa Roho. **Sasa tunapaswa kuelewa nguzo za imani yetu ni nini,—ukweli ambao umetufanya watu tulio, ukituongoza hatua kwa hatua**.

## Uzoefu wa Awali

Baada ya kupita kwa wakati wa 1844 tulichunguza Maandiko ili kupata ukweli kama hazina iliyositirika. Nilikutana na ndugu, na tukasoma na kuomba bila kukoma. Mara nyingi tulikuwa pamoja hadi usiku kabisa, na wakati mwingine hata usiku wote, tukiomba nuru na kuyachunguza maandiko. Mara kwa mara ndugu hawa walikuja pamoja kutafiti Bibilia, ili kwamba waweze kufahamu maana yake, na kuandaliwa kuifundisha kwa nguvu. Walipofikia pahali katika utafiti wao pa kusema, "Hatuwezi fanya lingine zaidi" Roho wa Bwana angekuja juu yangu. Ningechukuliwa katika maono, na maelezo wazi ya mafungu tuliyokuwa tukiyasoma yangetolewa kwangu, pamoja na maelezo ya jinsi tungetenda kazi na kufundisha kwa ufasaha. **Hivyo nuru ilitolewa ambayo ilitusaidia kuyafahamu maandiko *kuhusiana na Kristo*, huduma yake, na ukuhani wake. Msatari wa ukweli ukiendelea kutoka wakati huo hadi wakati ambao tutaingia katika mji wa Mungu, uliwekwa wazi kwangu, na nilipeana kwa wengine maagizo ambayo Bwana alikuwa amenipa**.

Katika wakati huu wote sikuweza kufahamu fikara za ndugu. Akili zangu zilikuwa zimefungwa, kama ilivyokuwa, na singefahamu maana ya maandiko tuliyokuwa tukisoma. Hii ilikuwa moja ya huzuni kuu ya maisha yangu. Nilikuwa katika hali hii ya mawazo hadi hoja kuu za imani yetu zilipowekwa wazi kwa mawazo yetu, kwa uiano na Neno la Mungu. Ndugu walijua kwamba, wakati siko kwenye maono, singeyafahamu masuala haya, na walikubali, kama nuru kutoka mbinguni, ufunuo uliotolewa.

Makosa mengi yalizuka, na ingawa wakati huo nilikuwa zaidi kidogo kuliko mtoto, nilitumwa na Bwana kutoka sehemu moja hadi nyingine kukemea wale ambao walishikilia mafundisho haya ya uongo. Kulikuwa na wale waliokuwa katika hatari ya kuingia katika ushabiki, na nilialikwa kwa jina la Bwana kuwapa maonyo kutoka mbinguni.

**Tutakutana na mafundisho haya haya ya uongo tena**. Kuna wale ambao watadai kuwa na maono. Mungu anapokupa ushahidi wazi kwamba maono yanatoka kwake, unaweza yakubali, lakini usiyakubali kwa ushahidi mwingine wowote; kwa sababu watu watapotoshwa zaidi na zaidi katika nchi za kigeni na Marekani. Bwana anataka watu wake waenende kama waume na wake wenye akili.

## Wokovu katika Ukweli

**Katika siku zijazo, udanganyifu wa kila aina utazuka, na tunataka pahali dhabiti pakuweka miguu yetu. Tunataka nguzo dhabiti za kujenga. Sio hata nukta moja itaondolewa kutoka kwa kile ambacho Bwana ameanzisha. Adui ataingiza ndani nadharia za uongo, mafundisho kama vile hakuna patakatifu.** ***Hii ni moja ya hatua ambayo kutakuwa na kuondoka kutoka kwa imani*****. Tutapata wapi usalama isipokuwa kwa ukweli ambao Bwana amekuwa akitoa katika miaka hamsini iliyopita?**

Wale ambao wanatafuta kuondoa alama za kale hawashikili; hawakumbuki jinsi wamepokea na kusikia. Wale ambao hujaribu kuleta nadharia ambazo zitaondoa **nguzo za imani yetu kuhusiana na patakatifu, au** ***kuhusiana na utu wa Mungu au wa Kristo***, wanatenda kama watu vipofu. Wanatafuta kuleta ukosefu wa hakika na kuwaweka watu wa Mungu katika kuyoyoma, bila nanga. {Ms62-1905.14}

**Ushuhuda wenyewe utakuwa** ***ufunguo*** ambao utaelezea ujumbe unaotolewa, **kama maandiko yanavyoelezewa na maandiko-** — Letter 73, 1903. {1SM 42.2} "Kuhusiana na ushuhuda, **hakuna chochote kimepuuzwa; hakuna chochote kimetengwa; lakini wakati na mahali lazima vizingatiwe.** {1SM 57.2}

"Na sasa kwa wote walio na hamu ya ukweli nitasema: usiisikilize habari ambayo haijathibitishwa kuhusu kile ambacho Dada White ametenda **au kusema** au kuandika. **Kama unataka kujua kile ambacho Bwana amedhihirisha kupitia kwake; soma kazi yake iliyochapishwa**. Kuna sehemu zozote za hisa kuhusiana na kile ambacho hajaandika, usiziongeze kwa shauku na kuripoti uvumi kwa kile ambacho amesema. {5T 696.1}

## Ushuhuda wa Waanzilishi wa Uadventista

Wengi wa watu wetu hawatambui **jinsi misingi ya imani yetu imewekwa imara. Mume wangu, Mzee Joseph Bates, Baba Pierce, Mzee [Hiram] Edson, na wengine ambao walikuwa makini, wazuri, na wa kweli, walikuwa baadhi ya wale ambao, baada ya kipindi cha 1844 kupita, walitafiti ukweli wa hazina iliyositirika.** Nilikutana nao, na tukasoma na kuomba bila kukoma. Mara nyingi tulikuwa pamoja hadi usiku kabisa, na wakati mwingine hata usiku wote, tukiomba nuru na kuyachunguza maandiko. Mara kwa mara ndugu hawa walikuja pamoja kutafiti Bibilia, ili kwamba waweze kufahamu maana yake, na kuandaliwa kuifundisha kwa nguvu. Walipofikia pahali katika utafiti wao pa kusema, "Hatuwezi fanya lingine zaidi" Roho wa Bwana angekuja juu yangu. Ningechukuliwa katika maono, na maelezo wazi ya mafungu tuliyokuwa tukiyasoma yangetolewa kwangu, pamoja na maelezo ya jinsi tungetenda kazi na kufundisha kwa ufasaha. Hivyo nuru ilitolewa ambayo ilitusaidia kuyafahamu maandiko kuhusiana *na* ***Kristo*****,** huduma yake, na ukuhani wake. **Msatari wa ukweli ukiendelea kutoka wakati huo hadi wakati ambao tutaingia katika mji wa Mungu, uliwekwa wazi kwangu,** na nilipeana kwa wengine maagizo ambayo Bwana alikuwa amenipa." {E. G. White, Selected Messages Book 1, pp. 206, 207. 1904}

**Msatari wa ukweli ukiendelea** kutoka wakati huo hadi wakati ambao tutaingia katika mji wa Mungu, uliwekwa wazi kwangu, na nilipeana kwa ndugu na dada maagizo ambayo Bwana alikuwa amenipa. **Walijua kwamba, wakati siko kwenye maono, singeyafahamu masuala haya**, na walikubali, kama nuru kutoka mbinguni, ufunuo uliotolewa kwangu. **Kwa hivyo hoja zinazotuongoza katika imani yetu kama tunavyozishikilia leo ziliwekwa imara. Hoja baada ya nyingine ilielezewa wazi, na ndugu wote wakawa na uiano**. {Lt253-1903.4}

**Kusanyiko lote la waumini liliunganishwa katika kweli**. Kuna wale ambao walikuja na mafundisho ya ajabu, lakini hatukuogopa kukutana nao. Uzoefu wetu ulikuwa **umejengeka kwa njia ya ajabu kwa ufunuo wa Roho Mtakatifu**. {Lt253-1903.5}

Kama watu, **tunafaa kusimama imara juu ya jukwaa la ukweli wa milele**

ambao umepitia majaribio na ukapita. Tunapaswa kushikilia **nguzo dhabiti za imani yetu. Kanuni za kweli ambazo Mungu amedhihirisha kwetu ndizo msingi wetu wa kweli tu. Zimetufanya jinsi tulivyo. Mabadiliko ya wakati hayajapunguza thamani yake. Ni juhudi za mara kwa mara za adui kuondoa ukweli huu katika muktadha wake, na kuweka nadharia za kuyumba pahali pake. Ataleta** kila kitu ambacho anaweza ili kutekeleza mpangilio wake potofu. **Lakini Bwana atainua watu wenye mtazamo makini, ambao wataupa ukweli huu pahali pake sahihi katika mpango wa Mungu**. {SpTB02 51.2, 1904}

**Hakuna msatari wa ukweli ambao umewafanya Waadventista wa Sabbato jinsi walivyo utadunishwa. Tunazo alama za kale**, uzoefu, na wajibu, **na tunapaswa kusimama imara katika kutetea kanuni zetu**, kwa mtazamo mzima wa ulimwengu. {6T 17.2}

Jumbe za kila mpangilio na namna zimewekwa juu ya Waadventista wa Sabbato, **kuchukua nafasi ya ukweli ambao, hoja baada ya nyingine, imechunguzwa kupitia kwa utafiti wa maombi, na kudhibitishwa kuwa utendaji wa muujiza wa Bwana**. Lakini **alama ambazo zimetufanya jinsi tulivyo, zinastahili kudumishwa**, na **zitadumishwa**, kama Mungu alivyosababisha kupitia Neno lake na ushuhuda wa Roho wake. Anatuita kushikilia kwa nguvu, pamoja na imani dhabiti, **kanuni za msingi ambazo zimewekwa juu ya utawala ambao hauna shaka**. {1SM 208.2}

Rekodi ya yale ambayo watu wa Mungu walipitia **katika historia ya awali ya kazi yetu lazima ichapishwe upya**. Wengi wa wale ambao wameingia katika ukweli tangu wakati huo **hawajui njia ambayo Bwana aliifanya. Kile ambacho William Miller na washirika wake walipitia, ya Captain Joseph Bates, na waanzilishi wengine katika ujumbe wa Uadventista lazima yawekwe mbele kwa watu wetu.** Kitabu cha Mzee Loughborough lazima kipewe makini. Viongozi wetu wanapaswa kuona kile kinachoweza kufanywa ili kusambazwa kwa kitabu hiki. {Lt105-1903.4}

Mzigo wa kuonya ambao sasa utakuwa kwa watu wa Mungu, karibu zaidi, ni **ujumbe wa malaika wa tatu**. Na wale ambao wanatafuta kuelewa ujumbe huu **hawataongozwa na Mungu kuweka katika kazi Neno ambalo litadunisha misingi na kuondoa nguzo za imani ambayo imewafanya**

**Waadventista wa Sabbato jinsi walivyo leo**. Ukweli ambao umekuwa ukijifunua kwa mpangilio wake, kama tunavyoendelea katika mstari wa unabii unaodhihirishwa katika Neno la Mungu, ni ukweli, takatifu, ukweli wa milele leo. Wale ambao walipitia juu ya ardhi hatua kwa hatua katika historia iliyopita ya uzoefu wetu, wakiona mtiririko wa ukweli katika unabii, waliandaliwa kukubali na kutii kila mwali wa mwanga. Walikuwa wakiomba, kufunga, kutafiti, na kuchunguza ukweli kama hazina iliyostirika, na Roho Mtakatifu, tunajua, alikuwa akitufundisha na kutuongoza. {Ms31-1896.9}

**Katika siku zijazo, udanganyifu wa kila aina utazuka, na tunataka pahali dhabiti pakuweka miguu yetu. Tunataka nguzo dhabiti za kujenga. Sio hata nukta moja itaondolewa kutoka kwa kile ambacho Bwana ameanzisha.** *Adui ataingiza ndani nadharia za uongo, mafundisho kama vile hakuna patakatifu. Hii ni moja ya hatua ambayo kutakuwa na kuondoka kutoka kwa imani.* **Tutapata wapi usalama isipokuwa kwa ukweli ambao Bwana amekuwa akitoa katika miaka hamsini iliyopita**? {RH May 25, 1905, par. 28}

**Wakati nguvu za Mungu zinashuhudia ukweli ni nini, kwamba ukweli utasimama milele kama ukweli. Hakuna dhana ya baadaye, kinyume cha nuru ambayo Mungu ametoa inapaswa kukubaliwa**. {Lt329-1905.17}

**Watu watazuka** na tafsiri za maandiko ambazo ni ukweli kwao, lakini ambazo sio ukweli. **Ukweli wa wakati huu, Mungu ametupa kama msingi wa imani yetu**. Yeye mwenyewe ametufundisha ukweli ni nini. *Mmoja atainuka, na mwingine pia, na nuru ambayo ni kinyume na nuru ambayo Mungu ametupa chini ya onyesho la Roho Mtakatifu.*

**Wachache bado wako hai ambao walipitia uzoefu uliopatikana katika kuanzisha ukweli huu. Mungu kwa neema amehifadhi maisha yao yajirudie rudie hadi mwisho wa maisha yao**, uzoefu waliopitia hata kama Yohana alipitia hadi mwisho wa maisha yake. **Na wabeba-kiwangogezi ambao wameanguka katika kifo, watazungumza kupitia kwa kuchapishwa upya kwa hati zao. Ninaelekezwa kwamba kwa hivyo sauti zao zitasikika. Watabeba ushahidi wao wa kile kilicho ukweli wa wakati wa sasa**. {Lt329-1905.18}

**Hatupaswi kupokea maneno ya wale ambao wanakuja na ujumbe ambao unakinzana na hoja za kipekee za imani yetu**. Hukusanya na kuweka pamoja mafungu mengi kama idhibati ya nadharia zao potovu. **Hili limefanywa tena na tena katika miaka hamsini iliyopita**. Na **ingawa maandiko ni Neno la Mungu, na yanafaa kuheshimiwa, matumizi yake, kama matumizi haya yanaondoa nguzo moja ya msingi ambao Mungu amedumisha miaka hii hamsini, ni kosa kubwa**. **Yule ambaye hufanya matumizi kama hayo hajui udhihirisho wa ajabu wa Roho Mtakatifu ambaye alitoa nguvu na msukumo kwa ujumbe uliopita ambao umekuja kwa watu wa Mungu**. {Lt329-1905.19}

**Wacha ukweli usipoteze mtazamo uliopita ambao washindani hawa wasiochoka** waliweka kando kila kitu ili kukuza kazi hiyo. **Ukweli kwamba wamezeeka na kuwa jivu katika hudumu ya Mungu sio sababu yao kukoma kufanya athari kuu kuwaathiri wanadamu ambao wana maarifa kidogo zaidi ya kazi na uzoefu mchache zaidi katika mambo ya uungu**. Ingawa wamechoka na hawawezi kubeba mzigo mzito ambao watu wachanga wanaweza na wanapaswa kubeba, thamani yao kama washauri ni ya kwanza. **Wamefanya makosa, lakini wamejifunza hekima kutoka kwa kuanguka kwao; wamejifunza kuepuka kosa na hatari, na kwa hivyo hawana uwezo wa kutoa mashauri yenye hekima**? Wametiwa katika majaribu na hukumu, na, ingawa wamepoteza baadhi ya nguvu zao, hawapaswi kuwekwa kando na watu wenye uzoefu mdogo, ambao wanajua machache sana kuhusu kazi na kujikana nafsi kwa waanzilisjhi hawa. **Mungu kwa hivyo hawaweki kando. Anawapa neema ya kipekee na maarifa.** {7T 287.3}

Wachache wa **viongozi wakongwe wa kuweka kiwangogezi** bado wanaishi. Ninatamani kwa hamu sana kwamba ndugu na dada zetu **wa waheshimu na kuwapa sifa njema waanzilishi hawa**. Tunawawasilisha mbele yenu kama watu ambao wanajua majaribu ni nini. Nimeagizwa kusema, **kila muumini na awaheshimu watu ambao walifanya sehemu maarufu wakati wa siku za awali za ujumbe, na ambao wamepitia majaribu na magumu na ufukara mwingi**. Watu hawa wamezeekea katika huduma. Sio kitambo sana, watapokea zawadi yao. {Lt47-1902.12}

Wale ambao walipitia hali hii wanapaswa kuwa imara kama mwamba

kwenye kanuni ambazo zilitufanya Waadventista wa Sabbato. Wanapaswa kuwa watenda kazi pamoja na Mungu, wakifungamanisha ushuhuda na kutia muhuri sheria miongoni mwa wanafunzi wake. **Wale ambao walikuwa katika kuanzisha kazi yetu juu ya msingi wa ukweli wa Bibilia; wale ambao wanajua alama ambazo zimeonyesha njia sawa wanafaa kurejelewa kama watenda kazi wa thamani kuu**. Wanaweza zungumza kupitia kwa uzoefu binafsi, kuhusiana na ukweli waliopewa. Watu hawa hawapaswi kuruhusu imani yao kubadilishwa kwa ukafiri; **hawataruhusu bendera ya malaika wa tatu iondolewe mikononi mwao**. Watashikilia mwanzo wa ujasiri wao kwa nguvu hadi mwisho. **Bwana ametangaza kwamba historia ya mambo yaliyopita itapitiwa tunapoingia katika kazi ya mwisho. Kila ukweli ambao ametoa kwa siku hizi za mwisho utatangazwa kwa ulimwengu. Kila nguzo ambayo ameianzisha itafanywa imara. Sasa hatuwezi enda kando ya msingi ambao Mungu ameanzisha**. Sasa hatuwezi ingia kwa mpangilio mpya; kwa sababu hili litamaanisha kuasi kutoka kwa ukweli. {Ms129-1905.6}

Namshukuru sana Baba yangu wa mbinguni kwa wema na fadhili kuu ambazo hunipa kila siku... akili yangu inawaza zaidi sasa kuhusu jitihada ya kuwasilisha kwa njia bora **ukweli kuhusiana na uzoefu wetu wa kwanza katika kutangaza ukweli ambao tunashikilia. Sitaki kupuuza au kuondoa kiungo kimoja katika mtiririko wa ushahidi ambao uliundwa kama, baada ya kipindi cha 1844 kupita**, kundi ndogo la watafutaji wa ukweli lilikutana kutafiti Bibilia na kumuomba Mungu nuru na mwongozo. Tulipoyachunguza maandiko kwa wingi wa maombi, ushahidi mwingi ulipeanwa kwetu kwa udhihirisho wa nguvu za Roho Mtakatifu. Ni umuhimu upi wa kina ulikuwa umewekwa kwa kila ushahidi ambao Mungu alitupa! Ukweli, hoja baada ya nyingine, iliwekwa imara katika mawazo yetu kwa udhabiti zaidi kwamba hatuwezi shuku. {Lt38-1906.1}

Wake kwa waume walikuja kutoka sehemu tofauti hadi ambapo mkutano ulikuwa umepangiwa kufanyika, kuona kama hawawezi kuleta nadharia zao za uongo. Lakini ingawa wangekuza makosa na wakati mwingine mafundisho ya ushabiki, tulikuwa na ukweli uliokuwa dhabiti mawazoni mwetu kwamba hatukuwa na chochote cha kuogopa. {Lt38-1906.2}

**Ukweli tuliopewa baada ya kupita kwa kipindi cha 1844 ni *yakini* na**

***hauwezi badilika* kama wakati ambao Bwana alipotupa katika jibu kwa maombi yetu ya dharura**. Maono ambayo Bwana amenipa ni ya ajabu sana kwamba tunajua kile ambacho tumekubali ndicho ukweli. Hili lilionyeshwa na Roho Mtakatifu. Nuru, nuru ya thamani kutoka kwa Mungu, ilianzisha sehemu kuu ya imani yetu kama tunavyoshikilia leo. **Na ukweli huu utadumishwa katika mawazo yetu.** Lazima tuamke kutoka katika hali ya uvuguvugu, katika kuwa si baridi wala moto. Tunahitaji imani zaidi na kutumaini kwa Mungu zaidi. Hatupaswi kutosheka na kusalia tulipo. Lazima tuendelee hatua kwa hatua, kutoka kwa nuru hadi kwa nuru zaidi. {Lt50-1906.3}

Nimekuwa na wasilisho kuhusiana na uongo ambao Shetani anaingiza ndani wakati huu. Nimeagizwa kwamba **tunapaswa kufanya maarufu ushuhuda wa baadhi ya watenda kazi wakongwe ambao sasa wamekufa. Wacha waendelee kuzungumza kupitia kwa makala yao kama yanavyopatikana katika nambari za awali za kurasa zetu. Makala haya sasa yatachapishwa upya, ili kuwe na sauti hai kutoka kwa shahidi wa Bwana. Historia ya uzoefu wa kwanza katika ujumbe itakuwa nguvu ya kushinda ujuzi wa werevu wa uongo wa Shetani. Maagizo hayo yamerudiwa hivi karibuni. Lazima niwasilishe mbele ya watu ushuhuda wa Ukweli wa Bibilia na kurudia ujumbe teule uliotolewa miaka iliyopita**. Natamani kwamba mahubiri yangu yaliyotolewa kwenye mikutano ya makambi na katika makanisa yadumu na yatende kazi yake teule. {Lt99-1905.7}

## Joseph Bates

(1792 – 1872)

Wazazi wangu walikuwa washiriki wenye msimamo dhabiti kwa muda mrefu katika kanisa la jamaa (Congregational church), pamoja na watoto wao wote walioongolewa wakati huo, walitarajia kwa hamu kwamba pia tutaunganika nao. Lakini walikumbatia baadhi ya hoja katika imani yao ambazo sikuweza kuzielewa. Nitataja mbili tu: mbinu ya ubatizo wao, **na fundisho la utatu**. Baba yangu, ambaye alikuwa shemasi mwenye msimamo kwa muda pamoja nao, alifanya kazi kunishawishi kwamba walikuwa sawa katika hoja za mafundisho. Nilimwarifu kwamba mawazo yangu yalikuwa yanasubuliwa kuhusiana na ubatizo. Nilisema, "nilikusikia ukibatiza hadi watoto wachanga." Nilijibu, kwamba hayo yote yanaweza kuwa na imani yake; lakini Bibilia ilifundisha kwamba lazima kwanza uamini na kisha

ubatizwe (Marko 16:16;1 Petro 3:21), lakini sikuwa na uwezo wa kuamini nilipokuwa mtoto mchanga. **Kuheshimu utatu, nilihitimisha kwamba ni jambo lisilowezekana kwangu kuamini kwamba Bwana Yesu Kristo, Mwana wa Baba, bado alikuwa Mungu Mwenyezi, Baba, mmoja na kiumbe sawa. Nilimwambia Baba yangu, "Kama unaweza nifanya niamini kwamba tuko sawa katika hali hii, kwamba wewe ni baba yangu, na mimi mwanao; na kwamba bado mimi ni Baba yako, na wewe ni mwanangu, basi nitaamini utatu (trinity)**." {AJB 204.2, 1868}

Jambo moja zaidi: kuzomewa zaidi kunatolewa kwa wale wa kundi letu ambao wamejiunga na Wayumbishaji. Nasema kwamba ni aibu kwao kwanza, kuhubiri kwa uazi na kwa kipekee kuja kwa Bwana wetu Yesu Kristo mwenyewe kwa haraka kuwakusanya watakatifu – na kisha kuenda na kujiunga na Wayumbishaji katika imani yao, kwamba yeye (Yesu) alikuja kiroho katika Mama yao, Ann Lee, zaidi ya miaka sabini iliyopita. **Hili, bila shaka yoyote akilini mwangu, linahusiana na somo lao la awali na fundisho liitwalo utatu. Unawezaje pata hatia katika imani yao wakati ambao unafundisha kile ambacho wanafundisha hasa, haiwezekani – hapana haiwezekani kueleweka, fundisho**?...{SC3 187.1}

**Tunaamini kwamba Petro na Bwana wake walisuluhisha swali hili zaidi ya kuwa na mgogoro, Mathayo 16:13-19;** na siwezi ona ni kwa nini Danieli na Yohana hawajadhibitisha kikamilifu **kwamba Kristo ni Mwana, na, sio Mungu Baba**. Danieli anawezaje elezea maono yake ya sura ya 7, Kama "Kristo alikuwa Mungu." **Hapa anaona mmoja "kama Mwana" (na haiwezi thibitishwa kwamba ilikuwa mtu mwingine yeyote) wa Adamu, na akapewa Mamlaka, na Utukufu, na Ufalme;" na mzee wa siku. Kisha Yohana anaelezea mmoja akiketi kwenye kiti cha enzi na kitabu katika mkono wake wa kulia, na kwa usahihi aliona Yesu akija kwenye kiti cha enzi na akachukua kitabu kutoka mikononi mwa yule aliyekuwa ameketi pale. Sasa kama inawezekana kufanya shughuli hizi mbili tofauti kabisa kuonekana katika mtu mmoja, basi naweza amini kwamba Mungu alikufa na akazikwa badala ya Yesu, na kwamba Paulo alikosea aliposema, "Sasa Mungu wa amani alimfufua Bwana Yesu mchungaji mkuu wa kondoo**" nk., na kwamba Yesu hakumaanisha alichosema alipodai kwamba alitoka kwa Mungu, na alikuwa akienda kwa

Mungu, nk, nk,; na mengi zaidi, ikibidi, kuthibitisha mkanganyiko unaozuka kutoka kwa imani kama hiyo. {SC3 188.1}

## Roswell Fenner Cottrell

(1814 – 1892)

Watu wameenda kinyume mno katika kujadili fundisho la Utatu (Trinity). **Baadhi wamemfanya Kristo mwanadamu wa kawaida, akianza uwepo wake katika kuzaliwa kwake Bethlehemu; wengine hawajaridhishwa na kumfahamu kuwa kile ambacho Maandiko yanadhihirisha kwa uwazi, Mwana wa Mungu aliyekuwepo kabla, lakini amemfanya 'Mungu Baba' wake mwenyewe…** naweza shauri tu wale wote ambao wanampenda Bwana na Mkombozi wetu Yesu Kristo, kuamini yote ambayo Bibilia inasema kumhusu, na sio kingine zaidi…. **Tunaelewa kwamba istilahi utatu inamaanisha muunganiko wa watu watatu, sio ofisi, katika Mungu mmoja; ili kwamba Baba, Mwana na Roho Mtakatifu, angalau ni watatu, na mmoja zaidi. Kwamba mtu mmoja na watu watatu, na kwamba watu watatu ni mtu mmoja tu, fundisho ambalo tunatangaza ni kinaya kwa mantiki na akili.** Utu na sifa za Mungu ni juu zaidi ya kufikiwa na akili zangu na mantiki, ingawa naziamini: **lakini fundisho ambalo nakataa ni kinyume, ndio, hilo ndilo Neno, kwa kila akili na mantiki ambayo Mungu mwenyewe ameweka ndani yetu.** Fundisho kama hilo hatuagizi kuliamini. … **Lakini Muumbaji wetu amefanya kuwa mkanganyiko kwetu kwamba mtu mmoja anaweza kuwa watu watatu, na watu watatu ila mtu mmoja;** na katika neno lake alilodhihirisha hajatwagiza kuamini hivyo. Hili rafiki zetu wanafikiria linaweza pingika…

**Lakini kushikilia fundisho la Utatu sio ushahidi zaidi wa nia ovu ya kulevyo kwa mvinyo ambao mataifa yote yamekunywa. Ukweli kwamba hili lilikuwa moja ya mafundisho ambayo yaliongoza, kama sio lililokuwa kuu hasa, ambalo Askofu wa Rumi aliinuliwa kwa mfumo wa Papa, mengi hayasemwi kwa faida yake. Hili linaweza wafanya watu kutafiti wao wenyewe; kama wakati ambao roho ya Shetani akitenda miujiza hufanya utetezi wa nafsi kutokufa kabisa. Kama singekuwa nimeshuku awali, sasa ningekuwa nimeshikilia hadi mwisho, kwa neno ambalo mizimu ya sasa (modern Spiritualism) wanaweka ambayo hayakuwako. … Ufunuo unaenda zaidi yetu; lakini hakuna wakati**

**wowote unaenda kinyume cha mantiki na akili sahihi.** Mungu hajadai, kama papa alivyofanya, kwamba anaweza wafanya "haki wasio haki," wala, **baada ya kutufundisha kuhesabu, hajatwambia kwamba hakuna tofauti kati ya nambari za umoja na wingi**. Wacha tuamini kile ambacho amedhihirisha, na tusiongeze chochote kwacho." {R. F. Cottrell, Review & Herald, July 6, 1869}

**"Anaendelea kuthibitisha kwamba "mwanadamu nikiumbe wa utatu." Mwenye mwili, nafsi na roho. Kamwe sikusikia Mwanafunzi akikiri imani katika fundisho la utatu;** lakini mbona, kama mtu yuko na watu watatu katika mtu mmoja? Hasa, kwa vile mtu aliumbwa kwa mfano wa Mungu? **Lakini mfano aliosema, ulikuwa usawa wa maadili. Kwa hivyo mtu anaweza kuwa kiumbe wa utatu bila kuthibitishwa kwamba Mungu ndivyo alivyo. Lakini anamaanisha kwamba mtu mmoja ni watu watatu? Naweza sema kwamba mti una mwili, ngozi na matawi, na hakuna yeyote ambaye atapinga. Lakini kama nitathibitisha kwamba kila mti uko na miti mitatu, madai hayo yatashukiwa na baadhi ya watu.** Lakini kama wote walikubali kwamba mti mmoja ni miti mitatu, basi naweza thibitisha kwamba kulikuwa na miti tisini kwenye bustani langu, ambayo mtu hawezi hesabu ila thelathini. Naweza endelea na kusema, niko na miti tisini katika bustani yangu, na kwa vile kila mti una miti mitatu, niko na miti mia mbili na sabini. Hivyo kama mtu mmoja ni watu watatu, unaweza mpiga mara na tatu mara nyingi utakavyo." {R. F. Cottrell, Review & Herald, Nov. 19, 1857}

"Msimamo wa Waanzilishi wa SDA kuhusu Utatu

**Hili limekuwa fundisho maarufu likichukuliwa kuwa Orthodoxi tangu askofu wa Roma aliinuliwa kwa upapa kwa nguvu zake. Inachukuliwa kuwa uzushi hatari kulikataa; lakini kila mtu anaruhusiwa kuelezea fundisho hili kwa njia yake mwenyewe. Wote wanaonekana kufikiria kwamba lazima waishikilie, lakini kila mmoja yuko na uhuru kamili wa kuchukua njia yake ya kupatanisha viwakilishi vyake kinzani; na kwa hivyo mitazamo mingi inashikiliwa kulihusu na rafiki zake, wote wakiwa orthodoxi, nadhani, kwa vile kwa jina wanatia saini kwa fundisho hili.** Kwangu binafsi, sijawahi hisi kamwe wito wa kulielezea, wala kulipokea au kulitetea, wala sijawahi hubiri dhidi yake. Lakini labda ninaweka makadirio makubwa kwa Bwana Yesu Kristo kama wale ambao wanajiita Wautatu. Hii

ndio mara ya kwanza nimewahi chukua kalamu kusema chochote kuhusiana na fundisho hilo. Sababu zangu za kutolipokea na kulitetea, ni 1. **Jina lake sio la Maandiko. Utatu, au Mungu watatu, haujulikani na Bibilia; na nimekaribisha wazo kwamba mafundisho ambayo huhitaji maneno yameundwa na akili za mwanadamu, yenyewe na mafundisho ya kuundwa.** 2. **Sijawahi hisi wito wa kupokea na kuelezea ambacho ni kinyume cha mantiki na maana yote ambayo Mungu amenipa**. Majaribio yangu yote ya kuelezea suala kama hilo hayatakuwa wazi kwa rafiki zangu. Lakini kama naweza ulizwa kile ambacho ninafikiria kumhusu Yesu Kristo, jibu langu ni, ninaamini yote ambayo Maandiko yanasema kumhusu. **Kama ushuhuda unamwakilisha akiwa na utukufu pamoja na Baba kabla ya ulimwengu kuwepo, ni naamini hivyo. Kama imesemwa alikuwa na Mungu hapo mwanzo, kwamba alikuwa Mungu, kwamba vitu vyote viliumba naye na kwa yeye, na kwamba bila yeye chochote hakikumbwa ambacho kiliumbwa, ninaamini hivyo. Kama maandiko yanasema ni Mwana wa Mungu, ninaamini hivyo. Kama imetangazwa kwamba Baba alimtuma Mwanawe ulimwenguni, ninaamini alikuwa na Mwana wa Kutuma. Kama ushuhuda unasema yeye ni mwanzo wa uumbaji wa Mungu, ninaamini hivyo. Kama inasemwa kuwa mng'ao wa utukufu wa Baba, na mfano halisi wa nafsi yake, ninaamini hivyo. Na Yesu anaposema, 'Mimi na Baba yangu tu wamoja,' ninaamini hivyo; na anaposema, 'Baba yangu ni mkuu kuniliko,' ninaamini hivyo pia; ni neno la Mwana wa Mungu, na zaidi ya hili kuna busara kamili na ushahidi binafsi unaoonekana.**

**Kama nikiulizwa jinsi Baba na Mwana walivyo wa moja, ninajibu, Ni wamoja katika mantiki sio kinyume na maantiki. Kama sentensi inamaanisha chochote, Baba na Mwana ni viumbe wawili. Ni wa moja kwa maantiki sawa ambayo Yesu aliomba kwamba wanafunzi wake wawe na umoja. Lugha yake ni kwamba, kwamba waweze kuwa na umoja, "kama tulivyo na umoja." Inaweza pingwa, kama Baba na Mwana ni viumbe wawili tofauti, kwa kumuabudu Mwana na kumuita Mungu, hauvunji amri ya kwanza ya Sheria? Hapana; ni mapenzi ya Baba kwamba wanadamu wote wamheshimu Mwana, kama wanavyo mheshimu Baba. Hatuwezi ivunja amri na kukosa kumheshimu Mungu kwa kumtii. Kwa habari za Mwana Baba anasema, malaika wote wa**

**Mungu na wamsujudu. Malaika wakikataa kumwabudu Mwana, watakuwa wameasi dhidi ya Baba. Wana hurithi jina la Baba yao. Mwana wa Mungu kwa urithi amepewa jina bora zaidi kuliko malaika. Jina hilo ni jina la Baba yake.** Lakini kwa habari za Mwana Baba asema, "Kiti chako cha enzi, Ee Mungu, kitadumu milele na milele." Ebr. 1:8. Mwana anaitwa Mungu mwenyezi. Isa. 9:6. Na anapokuja ulimwenguni watu wake wamngojao watasema, Huyu ndiye Mungu wetu. Isa. 25:9. **Ni mapenzi ya Mungu kwamba tumheshimu Mwana. Kwa kufanya hivyo tunatoa heshima kuu kwa Baba. Tukikosa kumheshimu Mwana tunakosa kumheshimu Baba; kwa sababa anataka tumheshimu Mwanawe.**

Lakini ingawa Mwana anaitwa Mungu bado kuna Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo. 1 Pet. 1:3. Ingawa Baba anasema kwa Mwana, Kiti chako cha enzi, Ee Mungu, kitadumu milele na milele, bado kiti hicho cha enzi amepewa na Baba yake; na kwa sababu alipenda haki na kuchukia dhambi, anaendelea kusema, Mungu, Mungu wako, amekuweka juu ya wenzako. Ebr. 1:9. Mungu amemfanya huyu Yesu, ambaye ninyi mlimsulibisha, kuwa Bwana na Kristo. Matendo. 2:36. **Mwana ni Baba wa milele, sio wake mwenyewe, wala wa Baba yake, bali wa wanawe, lugha yake ni. Mimi pamoja na watoto Mungu alionipa.** Ebr. 2:13." {R. F. Cottrell, Review & Herald, June 1, 1869}

## Joseph Birchard Frisbie

(1816 – 1882)

"Mungu wa Jumapili.

Tutatoa dondoo chache, ili msomaji aone **tofauti pana kati ya Mungu wa Bibilia ikiletwa katika nuru kupitia kuitunza Sabbato, na mungu katika giza kupitia kutunza jumapili**. Katekismu ya Katoliki ikifupishwa na Rt. Rev. John Dubois, Askofu wa New York. Ukurasa 5. 'S. Mungu yuko wapi? Jibu. Mungu yuko kila mahali. S. Mungu anaona na kujua kila kitu? J. ndio, anajua na kuona vitu vyote...S. **Kuna Mungu wengi kuliko mmoja? J. Hapana kuna Mungu mmoja tu. S. kuna watu zaidi ya mmoja katika Mungu? J. Ndio; katika Mungu kuna watu watatu. S. Ambao ni? J. Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu. S. hakuna**

**Mungu watatu? J. hapana; Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ni mmoja na Mungu sawa'**...mawazo haya yana mkataba mzuri na wana-falsafa wa mataifa...**Tunapaswa kukosa kuamini kwamba Mungu wa Jumapili alitoka mahali ambapo utunzaji wa Jumapili ulitoka**." {J. B. Frisbie, Review & Herald, March 7, 1854, The Sunday God, Uk. 50}

"Kwa mujibu wa fundisho kwamba watatu hasa na Mungu wa milele ni Mungu mmoja tu, tunawezaje kupatanisha…Matendo [10:38]. "Jinsi Mungu alivyomtia Yesu mafuta kwa Roho Mtakatifu," &c. **Mtu wa kwanza anachukua nafasi ya mtu wa tatu na kumpaka mafuta mtu wa pili na akiwa kwa wakati mmoja pamoja naye yeye mwenyewe**.

"Kwamba watatu ni mmoja, na mmoja ni watatu, ni wazo ambalo hunishangaza;
Kwa wengi ni wahenga wenye elimu inasemwa kwamba watatu ni mmoja katika Uungu.
"Baba anaweza kuwa Mwana, kwa sababu wote pamoja hufanya mmoja;
Mwana vilevile anaweza kuwa Baba, bila badiliko hata ndogo kwa yeyote.
"Ndio, na Roho mbarikiwa awe Baba, Mwana na utatu;
Hii ni imani ya watu wa Kristo, Ambao hujiita Waorthodoxi wa kweli,
Yote ambayo ni dhidi ya akili ya kawaida wazi au tutoe kosa."
{J. B. Frisbie, Review & Herald, March 12, 1857}

## Joseph Harvey Waggoner

(1820 – 1889)

"***Wanatheologia wengi kwa kweli hudhani kwamba Upatanisho, kwa heshima na ufanisi wake, unakaa katika fundisho la Utatu: lakini tunakosa kuona uhusiano wote kati ya hayo mawili***. Kwa kinyume, watetezi wa fundisho hilo hakika walianguka katika utata ambao wanaonekana kuchoka kuuepuka. Utata wao unapatikana katika hili: ***wanachukulia kukataa Utatu sawa na kukataa uungu wa Kristo. Kama ni hivyo, tunapaswa kushikilia fundisho la utatu kwa ushupavu kadri mtu awezavyo; lakini sivyo***. *Wale ambao wamesoma maneno yetu juu ya kifo cha*

*Mwana wa Mungu wanajua kwamba tunaamini uungu wa Kristo kwa udhabiti; lakini hatuwezi kubali dhana ya utatu, kama inavyoshikiliwa na Wana-utatu, bila kuacha madai yetu juu ya heshima ya dhabihu iliyotolewa kwa ukombozi wetu.*" {J. H. Waggoner, *The Atonement in the Light of Nature and Revelation*, uk. 164, 165}

"*Tofauti kati ya Kristo na Mungu wa kweli inawekwa wazi kabisa na maneno ya Mkombozi mwenyewe katika Yohana 17:3*: "Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma." *Mkazo zaidi unawekwa kwa Isa. 9:6, kama ikithibitisha utatu*, ambayo tumenukuu awali, ikirejelea Kuhani wetu Mkuu ambaye alimwaga damu yake kwa ajili yetu. Waasisi wa nadharia hii watasema kwamba inarejelea utatu kwa sababu Kristo anaitwa Baba wa milele. *Lakini kwa sababu hii, na zingine, tunathibitisha kwamba haiwezi kuwa* ***inarejelea utatu***. Kristo ni Baba katika Utatu? Kama ndivyo, yeye ni Mwana kwa njia gani? Ama kama yeye ni wote kunawezaje kuwa aje na utatu? Kwa kuwa utatu ni watu watatu. Kukubaliana na utatu, tofauti kati ya Baba na Mwana lazima iwekwe kando. Kristo anaitwa "mtu wa pili katika utatu," lakini kama fungu hili linathibitisha utatu, ama lina urejelea kabisa, linathibitisha kwamba sio wa pili, bali wa kwanza. Na kama ni wa kwanza, wa pili ni nani? Ni wazi kabisa kwamba fungu hili halirejelei fundisho kama hilo." {J. H. Waggoner, *ibid*, uk. 168, 169}

"Imani ya Athanasia ('Athanasian creed')... ilianzishwa na kuelezewa na Athanasius. Kabla ya wakati huo hakukuwa na popote na mshikamano wa imani. *Wengi wa waandishi wa awali wamekuwa wana-falsafa wa kipagani, ambao kufikia mawazo ya tabaka hilo, mara nyingi kulihitaji jitihada dhabiti kuthibitisha kwamba kulikuwa na kuchanganya mifumo hiyo miwili, Ukristo na falsafa. Kuna kazi nyingi za uandishi wao za kutetea msimamo huu.* Bingham anazungumza kuhusu mitazamo isiyoeleweka inayoshikiliwa na baadhi kwa maneno yafuatayo muhimu: "'kuna baadhi ambao walibadilisha fundisho la Utatu kuwa Mungu wa tatu (***Tritheism)****, na, badala ya watu watatu watakatifu chini ya uchumi wa Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, walileta* ***viumbe watatu wenye asili sawa, mpangilio sawa, na wenye asili binafsi, wakiwafanya kuwa kanuni huru kabisa, bila uhusiano wowote wa Baba au Mwana, ambao ni dhana nzuri ya miungu tatu****. Na baada ya*

*kufanya mabadiliko haya katika fundisho la Utatu, walifanya badiliko lingine chini yake katika mbinu ya ubatizo.'*-Antiquities, kitabu 11, sura. 3, & 4. "Nani anaweza tofautisha aina hii ya usemi na ule ambao ulitolewa katika baraza la Constantinople katika A.D. 381, ambapo imani ya kweli inatangazwa kuwa ile ya "Utatu ambao haukuumbwa na wa kuimarika na wa milele pamoja?' *kweli ni kwamba tunapata wazo sawa ambalo linaelezewa hapa na Bingham likitawala katika uwandishi wa orthodox wa karne ya pili na ya tatu.* ***Hakuna 'uhusiano barabara kati ya Baba na Mwana'*** *unaopatikana katika maneno ya baraza, ambalo limenukuliwa hapo juu... Bingham anasema kosa hili kuhusiana na* ***Utatu wa viumbe wenye mpangilio sawa, asili binafsi na huru lilizuka kanisani mapema sana;*** *na kwa hivyo tunalipata katika waandishi wa awali baada ya kipindi cha mitume… Tunaliacha na uamuzi bora wa kila msomaji asiye na chuki kwamba* ***batizo tatu ni thabiti zaidi na dhana ya "viumbe watatu wenye asili sawa, mpangilio sawa, na wenye asili binafsi"****, kuliko dhana la ubatizo kwa jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, na kwa mfano wa kifo na kufufuka kwa Mkombozi.*" {J. H. Waggoner, *Thoughts on Baptism,* 1878}

"Kuna swali moja ambalo limetiwa utata zaidi katika ulimwengu wa theolojia ambalo hatujadhahania kuingilia. *Ni hilo la utu wa Roho wa Mungu*. Dhana zinazotawala za watu ni tofauti kabisa, ghafi mara nyingi, na neno linafahamika tofauti; hivyo umoja wa maoni juu ya hoja hii hauwezi tarajiwa hadi wote waweze kuelezea wazi kile ambacho wanamaanisha kwa neno, au hadi wote wakubali maana fulani moja ambayo itatumika kwa neno. Lakini kadri uiano huu haupo, inaonekana kwamba majadiliano ya suala hili hayawezi zaa matunda, hasa kwa vile sio swali la ufunuo wa moja kwa moja. *Tuko na haki ya kuwa na mwelekeo chanya kwa imani yetu na kauli zetu pekee wakati ambao maneno ya maandiko yako wazi kuleta suala katika kiwango cha ithibati chanya. Hatuko tu tayari mbali pia na hamu ya kuachia ambapo neno la Mungu linaachia.* ***Kutoka kwalo tunajifunza kwamba Roho wa Mungu ni uwezo wa kutisha na waajabu ambao hutoka kwenye kiti cha enzi cha ulimwengu, na ambaye ni muigizaji fanisi katika kazi ya uumbaji na ukombozi.****"* {J. H. Waggoner, *The Spirit Of God; Its Offices And Manifestations*, uk. 8, 9. 1877}

"***Kama ivyoelezewa awali, kosa kuu la Wana-utatu, katika kujadili suala***

***hili, ni hili: hawafanyi tofauti yoyote kati ya kukataa utatu na kukataa uungu wa Kristo. Huona tu miisho miwili, ambayo ukweli hukaa kati yake; na kuchukua kila kauli inayorejelea uwepo wa Kristo kabla kama ushahidi wa utatu. Maandiko kwa wingi hufundisha uwepo wa Kristo kabla na uungu wake; lakini yako kimya kabisa kuhusiana na utatu.*** Tangazo kwamba, Mwana mtakatifu wa Mungu hawezi kufa, liko mbali kutoka kwa mafundisho ya Bibilia kama giza ilivyo kutoka kwa nuru. Na tutawauliza wana-utatu, ni katika gani ya hali hizo mbili tunadaiwa kwa ukombozi? Jibu litakuwa, bila shaka, kwa yule ambaye alikufa au kumwaga damu yake kwa ajili yetu; kwa kuwa "tumekombolewa kwa damu yake." Basi ni dhahiri kwamba kama asili ya uanadamu tu ndio ilikufa, Mkombozi wetu ni binadamu tu, na Mwana mtakatifu wa Mungu hakuchukua sehemu yoyote katika kazi ya ukombozi, kwa sababu hangeteseka wala kufa. ***Kwa kweli, tunasema sawa, kwamba fundisho la utatu hudunisha Upatanisho,*** kwa kushusha dhabihu, damu ya kununuliwa kwetu, chini kwa kiwango cha Usocinianism." {J. H. Waggoner, *The Atonement In The Light Of Nature And Revelation*, pp. 173, 174}

"Swali. *Jumapili ni nini, au Siku ya Bwana kwa jumla?*

Jibu. ***Ni siku ambayo iliteuliwa na Mitume kwa heshima ya Utatu mtakatifu mno,*** na kwa ukumbusho kwamba Kristo Bwana wetu alifufuka kutoka kwa wafu siku ya Jumapili, alimtuma roho Mtakatifu Jumapili, &c.; na kwa hivyo inaitwa Siku ya Bwana. Pia inaitwa Jumapili kutoka kwa dhehebu la kale la Roma la Dies Solis, siku ya jua, ambayo ilikuwa wakfu kwalo. - *Douay Catechism*, Ukurasa 143." {J. H. Waggoner, *Review & Herald*, July 18, 1854}

## James Springer White
(1821 – 1881)

"MSIMAMO WA MASALIO

***Kama kosa la msingi, tunaweza orodhesha pamoja na sabbato hii ghushi makosa mengine ambayo Waprotestanti wametoa kwa kanisa la Katoliki,***

*kama kunyunyuziwa kwa ubatizo, utatu, fahamu za wafu na uzima wa milele katika taabu. Wengi ambao wameshikilia makosa haya ya imani, bila shaka wamefanya hivyo bila kujua;* ***lakini inaweza dhahaniwa kwamba kanisa la Kristo litabeba makosa haya hadi wakati mandhari ya hukumu yatakapoonekana juu ya ulimwengu? Tunadhani sivyo***. "Hapo ndipo penye subira ya watakatifu [katika ujumbe ambao unatolewa kabla ya Mwana wa Adamu kuchukua pahali pake katika wingu jeupe, Rev.xiv,14] wazishikao amri za Mungu na imani ya Yesu." *Kikundi hiki, ambacho kinaishi kabla ya marejeo ya pili, hakitakuwa kinashikilia tamaduni za watu, wala hakitakuwa kikishikilia makosa ya msingi yanayohusiana na mpango wa wokovu kupitia kwa Yesu Kristo.* ***Na jinsi nuru ya kweli inaangaza juu ya masuala haya, na wengi wanaikataa, ndivyo hukumu utakuja juu yao****. … Saa inayokaribia upesi, ya kutisha!***"** {J. S. White, *Review & Herald*, Septemba 12, 1854}

**"**Baba na Mwana walikuwa wamoja katika uumbaji wa mwanadamu, na katika ukombozi wake. *Alisema Baba kwa Mwana, "Natumfanye mtu kwa mfano wetu."* Na wimbo wa ushindi ambao waliokombolewa wanashiriki, ni kwa "Yule aketiye katika kiti cha enzi, na kwa Mwana-kondoo, milele na milele."**"** {J. S. White, *The Law and the Gospel*, uk. 1. 1870}

**"**Paulo anadhibitisha kwamba Mwana wa Mungu alikuwa katika umbo la Mungu, na kwamba alikuwa sawa na Mungu. 'Yeye ingawa alikuwa sawa na Mungu, hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho.' Flp. 2:6. Sababu ambayo sio wizi kwa Mwana wa Mungu kuwa sawa na Baba yake ni ukweli kwamba yeye ni sawa... ***Utatu ambao hauwezi elezeka ambao hufanya Uungu watatu ndani ya mmoja na mmoja ndani ya watatu, ni mbaya vyakutosha****; lakini ultra Unitarianism ambao humfanya Kristo dhaifu kwa Mungu ni mbaya zaidi. Mungu alisema kwa mtu dhaifu, "Natumfanye mtu kwa mfano wetu"?*" {J. S. White, *Review & Herald*, Novemba 29, 1877}

**"**Yesu aliomba kwamba wanafunzi wake wawe wamoja kama walivyokuwa wamoja na Baba yake. *Ombi hili halikutafakari mwanafunzi mmoja na vichwa kumi na viwili bali wanafunzi kumi na wawili, wakifanywa wamoja katika kitu na jitihada katika kazi ya bwana wao.* ***Wala Baba na Mwana si sehemu ya "watatu Mungu mmoja."*** *Ni viumbe wawili tofauti, ingawa*

*mmoja katika muundo na ukamilifu wa ukombozi.* Mwokovu, kuanzia wa kwanza kushiriki katika ukombozi mkuu, hadi wa mwisho, wote wanaonyesha heshima, na utukufu, na sifa, za ukombozi wao, kwa **wote Mungu** na **Mwna-kondoo**.**"** {J. S. White, *Life incidents*, uk. 343. 1868}

**"**Injili ya Mwana wa Mungu ni habari njema ya ukombozi kupitia Kristo. Mwanadamu alipoanguka, malaika walilia. Mbingu zilijawa na machozi. ***Baba na Mwna walishauriana, na Yesu alijitoa kuchukua mzigo wa mwanadamu aliyeanguka.*** Alijitoa kufa ili mwanadamu awe na uzima. *Baba alikubali kumtoa mpendwa wake wa pekee,* na habari njema ikaenea kote mbinguni, na duniani, kwamba njia ilikuwa imefunguliwa kwa ukombozi wa mwanadamu.**"**{J. S. White, *The Law and the Gospel*, uk. 2, 3. 1870}

**"**"Wapenzi, ingawa nilikuwa ninatamani sana kuwaandikia kuhusu wokovu ambao tunaushiriki sisi sote, niliona imenipasa kuwaandikia na kuwasihi kwamba mwishindanie IMANI iliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu…" (Yuda 3, 4) …Himizo la kushindania imani iliyokabidhiwa watakatifu, ni kwetu binafsi. *Na ni muhimu sana kwetu kujua ni kwa nini na nini tunashindania*. Katika fungu la 4 anatupa sababu ya kushindania IMANI, imani hasa; "kwa maana kuna watu," au kundi fulani ambalo hukataa Bwana Mungu wa pekee na Bwana wetu Yesu Kristo. … ***Njia ambayo watu wa kiroho wameelekea au kukataa Bwana Mungu pekee na Bwana Yesu Kristo mwanzo ni kutumia maneno Imani ya Utatu ya kale yasiyo kwenye maandiko***, viz., kwamba Yesu Kristo ni Mungu wa Milele, *ingawa hawana fungu moja la kuunga mkono hilo, wakati ambao tuko na maandiko wazi ya ushahidi mwingi kwamba ni Mwana wa Mungu wa milele.***"** {J. S. White, *The Day Star*, January 24, 1846}

**"***Baba alikuwa mkuu kumliko Mwana kwa kuwa alikuwa wa kwanza. Mwana alikwa sawa na Baba kwa kuwa alipokea kila kitu kutoka kwa Baba*.**"** {J. S. White, *Review & Herald*, January 4, ***1881***}

**"**Tunaambiwa na wale ambao hufundisha kukomeshwa kwa sheria ya Baba, kwamba amri za Mungu zinazotajwa katika Agano Jipya, sio zile kumi, mbali mahitaji ya injili, kama vile kuungama, imani, ubatizo na meza ya Bwana. Lakini kama hizi, na mahitaji mengine teule kwa injili, yote yanakumbatiwa

katika imani ya Yesu. Ni dhahiri kwamba amri za Mungu sio usemi wa Kristo na mitume wake. *Kuthibitisha kwamba usemi wa Mwana na Mitume wake ni amri za Baba, ni mbali kutoka kwa ukweli kama* ***uongo wa utatu wa kale*** *kwamba Yesu Kristo ndiye hasa na Mungu wa milele*. Na vile imani ya Yesu hukumbatia kila hitaji teule kwa injili, inafuata kwa umuhimu kwamba amri za Mungu, zinazotajwa na malaika wa tatu, zinakumbatia tu kanuni kumi za amri za Baba zisizobadilika kwa mpango wa yeyote, bali zinatumika kwa wote.**"** {J. S. White, *Review & Herald*, August 5, 1852}

**"***Ndugu. Cottrell anakaribia umri wa miaka thamanini, anakumbuka siku ya giza la mwaka wa 1780*, na amekuwa mtunza Sabbato kwa zaidi ya miaka thelathini. Awali alikuwa ameunganishwa na Seventh-Day Baptists, lakini katika sehemu fulani za mafundisho ametafautiana na mwili huo. ***Alikataa fundisho la utatu***, pia fundisho la ufahamu wa mwanadamu katikati ya kifo na ufufuo, na adhabu ya waovu katika fahamu za milele. Aliamini kwamba waovu wataangamizwa. Ndugu. Cottrell alimzika mkewe sio mbali tangu wakati huo, ambaye, inasemwa, alikuwa mmoja wa watu bora duniani. Sio kitambo sana tangu msafiri huyu apokee barua kutoka kwa marafiki kutoka Wisconsin, wakidai kuwa imetoka kwa M. Cottrell, mke wake, alalaye katika Yesu. Lakini yeye, akiamini kwamba wafu hawajui chochote, alikuwa tayari kukataa mara moja uzushi kwamba roho za watu, zijuazo kila kitu, hurejea na kuongea na waliohai. *Ukweli ni suala katika umri wake wa uzeeni*. Yuko na vijana watatu katika Mill Grove, ambao, pamoja na familia zao ni watunza Sabbato.**"** {J. S. White, *Review & Herald*, June 9, 1853}

**"*****Hapa tunaweza taja Utatu, ambao huondoa utu wa Mungu, na wa Mwanawe Yesu Kristo***, na wa kunyunyuzia au kumwagia badala wa "kuzikwa pamoja na Kristo katika ubatizo," "ukipandwa kwa mfano wa kifo chake:" *lakini tunapita kutoka kwa* ***visa*** kugundua kwamba mmoja ambaye anashikiliwa kuwa mtakatifu na karibu wote wanaojiita kuwa Wakristo, wote Wakatoliki na Waprotestanti. Ni, kubadilishwa kwa Sabbato ya amri ya nne kutoka siku ya saba hadi siku ya kwanza ya wiki.**"** {J. S. White, *Review & Herald*, Decemba 11, 1855}

**"SABABU ZA KATOLIKI KUTUNZA JUMAPILI.**

1. Kwa sababu "inaitwa Jumapili kutoka kwa dhehebu la kale la Roma la

Dies Solis, siku ya jua, ambayo ilikuwa wakfu kwalo." "Jumapili lilikuwa jina ambalo lilitolewa na mataifa kwa siku ya kwanza ya juma, kwa sababu ilikuwa siku ambayo waliabudu jua."

2. Kwa sababu ni "kwa heshima ya mbarikiwa Bikira Maria."

3. *Kwa sababu "ni siku iliyowekwa wakfu na mitume kwa heshima ya Utatu Mtakatifu zaidi.'"* {J. S. White, *Review & Herald*, April 4, 1854}

**"**"Ajabu ya dhambi" ilianza kutenda kazi kainsani katika siku za Paulo. Hatimaye ilijaza unyenyekevu wa injili, na ikaharibu fundisho la Kristo, na kanisa likaenda katika jangwa. Martin Luther, na wanamatengenezo wengine, waliinuka katika nguvu za Mungu, wakafanya hatua kuu zaidi katika matengenezo. ***Kosa kubwa ambalo tunaweza pata katika matengenezo ni, Wanamatengenezo waliacha kufanya matengenezo.*** *Kama wangendelea, na kuendelea zaidi, hadi kuacha masalia ya Upapa nyuma, mafundisho kama, umilele asilia, kunyunyuzia,* ***utatu****, na utunzaji wa Jumapili,* ***kanisa sasa lingekuwa huru kutoka kwa makosa yake yasiyo kwenye maandiko*****."** {J. S. White, *Review & Herald*, February 7, 1856}

**"**Kazi ya ukombozi, mafundisho na kwaongoza Waebrania ilipeanwa kwa yule ambaye anaitwa malaika. Kut.13:21; 14:19,24; 23:20-23; 32:34; Hes.20:16; Isa.63:9. Na malaika huyu Paulo anamwita "Mwamba wa kiroho ambao uliwafuata," na anadhibitisha, "kwamba Mwamba huo ulikuwa Kristo." 1Kor.10:4. *Baba wa milele kamwe haitwi malaika katika maandiko, wakati ambao yale malaika wamefanya mara nyingi yanahesabiwa kwa Bwana,* kwa vile ni wajumbe wake na wakala wa kukamilisha kazi yake. Inasemwa kumhusu ambaye aliwatangulia Waebrania kuwaokoa, "Jina langu liko katika yeye." *Katika matukio yote ya ajabu ya ukombozi huo mawazo ya* ***Yehova*** *yaliwakilishwa katika* ***Kristo*****."** {J. S. White, *Christ and the Sabbath*, uk. 11}

## Merritt E. Cornell

(1827 – 1893)

**"**Waprotestanti na Wakatolika karibu sana wameunganishwa katika hisia, kwamba sio vigumu kuelewa jinsi Waprotestanti watafanya sanamu kwa Mnyama. **Waprotestanti wengi huamini pamoja na Wakatoliki katika**

**Utatu**, kutokufa kwa nafsi, fahamu ya wafu, karama na adhabu katika kifo, mateso yasiyokuwa na mwisho ya waovu, urithi wa watakatifu juu mawinguni, kunyunyuziwa kwa ubatizo, na JUMAPILI YA KIPAGANI kwa Sabbato; **yote ambayo ni kinyume kwa roho na barua ya Agano Jipya.** Hakika kuna kati ya mama na binti, mfanano mkubwa sana wa familia.**"** {M. E. Cornell, Facts for the Times, uk. 76. 1858}

## John Nevins Andrews

(1829-1883)

**"**kila mshirika wa familia ya mwanadamu, isipokuwa Adamu, amekuwa na wazazi, na kila mmoja amekuwa na mwanzo wa siku; na kwa kweli, isipokuwa wawili, kila mmoja amekuwa na mwisho wa uzima. Hata malaika wa Mungu wote wako na mwanzo wa siku, ili kwamba watengwe kabisa na lugha hii kama washiriki wa familia ya wanadamu. *Na kama Mwana wa Mungu, atatengwa pia, kwa kuwa alikuwa na Mungu kama Baba yake, na alikuwa, katika sehemu fulani katika umilele, na mwanzo wa siku.***"** {J. N. Andrews, *Review & Herald*, September 7, 1869}

**"***Fundisho la Utatu ambalo lilianzishwa kanisani na baraza la Nice, A. D. 325.* ***Fundisho hili huharibu utu wa Mungu, na Mwanawe Yesu Kristo Bwana wetu.*** *Hatua zisizo maarufu ambazo zililazimishwa kwa kanisa ambazo zinaonekana katika kurasa za historia ya ecclesiastical vile vile zinaweza fanya kila muumini katika fundisho hilo kuaibika.***"** {J. N. Andrews, *Review & Herald*, March 6, 1855}

**"**Kwamba Mungu ni chemchemi na chanzo cha kuishi milele ni wazi kutoka kwa kauli ya Paulo. Kwa hivyo anazungumza kuhusu Mungu Baba: 'Yeye peke yake hapatikani na mauti, ambaye anakaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa, ambaye hakuna mwanadamu aliyemwona wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una Yeye milele; Amen.' 1 Tim. 6:16. *Fungu hili limeandikwa kwa ushahidi kufundisha Mungu anayejitegemea kuishi ni yeye pekee aliye, wake mwenyewe, yuko na asili hii ya ajabu.* Wengine wanaweza kuwa nayo ikitoka kwake, lakini yeye pekee ni chemchemi ya kuishi milele. "Bwana wetu Yesu Kristo ni chanzo cha uzima kwetu. 'Kama vile Baba alivyo na uzima ndani Yake, vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na uzima ndani Yake.' Yohana 5:26. 'Kama vile Baba aliye hai alivyonituma

Mimi, na kama nami ninavyoishi kwa sababu ya Baba, hivyo anilaye mimi ataishi kwa sababu yangu.’ Yohana 6:57. *Baba hutupa uzima katika Mwanawe.* ‘Huu ndio ushuhuda kwamba, Mungu ametupa uzima wa milele, nao huo uzima umo katika Mwanawe. Aliye naye Mwana wa Mungu anao uzima, yeye asiye na Mwana wa Mungu hana uzima.’ 1Yn 5:11,12. Maandiko haya yanaonyesha wazi kuwa Kristo ni chanzo cha uzima usio kuwa na mwisho, na wale tu walio nao na walio na Kristo.**”** {J. N. Andrews, *Review & Herald*, January 27, 1874 uk. 52}

## Changamoto ya Katoliki

**“**Waprotestanti hawaongozwi na Maandiko. [“Doctrinal Catechism”- uk. 101, 174, 351-355.]

“**S**. Kuna thibitisho lingine kwamba Waprotestanti hawaongozwi na Maandiko? **J**. Ndio; nyingi, kwamba hatuwezi kubali kiwakilishi kidogo katika kazi hii. Wanakataa mengi ambayo yako wazi katika maandiko, na kuhubiri mengi ambayo hayatambuliwi popote katika Kitabu hicho Kitakatifu.

**S**. Toa mfano wa yote? **A**. Wangekuwa, kama Maandiko ndio mtawala wao, wanatawadhana miguu, kulingana na amri ya Kristo, katika sura ya 13 ya Yohana mtakatifu; - wangekuwa wanaitunza, sio Jumapili, bali Jumamosi, kulingana na amri, ‘Ikumbuke siku ya Sabbato uitakase,’ kwa sababu amri hii, katika maandiko, haijabadilika au kuondolewa.”

“**S**. kuna njia nyingine ya kuthibitisha kwamba kanisa linauwezo wa kuweka tamasha za kanuni? **J**. Kama halingekuwa na uwezo huo, halingefanya hilo ambalo dini ya kisasa inakubaliana nalo; - halingebadilisha kuitunza Jumapili siku ya kwanza ya juma, kwa Jumamosi siku ya saba ya juma, badilisho ambalo halina mamlaka yoyote ya Maandiko.”

“***S****. mnatunza ukweli mwingine muhimu kama unavyo fundishwa na kanisa, ambao hauko wazi kwenye maandiko?* ***J****.* ***Fundisho la Utatu****, fundisho ambalo ufahamu hakika ni muhimu kwa wokovu,* ***halijawekwa waziwazi na dhahiri kwenye maandiko****, katika mtazamo wa Waprotestanti wa maelezo kibinafsi.***”** {*Review & Herald*, August 22, 1854}

# John Norton Loughborough

(1832 – 1924)

“SWALI KWA NDUGU. LOUGHBOROUGH.

NDUGU. WHITE: swali lifuatalo ningependa umpe, umtumie, Ndugu. Loughborough alielezee. W. W. GILES. *Toledo, Ohio.*

SWALI 1. *Ni pingamizi gani kubwa iliyoko katika fundisho la Utatu?*

JIBU. *Kuna pingamizi nyingi ambazo tunaweza himiza, lakini kwa sababu ya nafasi yetu ndogo tutazipunguza kuwa tatu zifuatazo:* ***1. Ni kinyume kwa akili za kawaida. 2. Ni kinyume na maandiko. 3. Asili yake ni Pagani na Uwongo.*** Nafasi hiz tutazielezea kwa kifupi kwa mpangilio wao. Na *1. Hakuna uiano kabisa na akili za kawaida kuzungumza kuhusu watatu kuwa mmoja, na mmoja kuwa watatu. Au kama baadhi wanavyoiweka, wakimuita Mungu “Mungu wa Utatu” au “watatu-Mungu-mmoja.”* ***Kama Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu kila mmoja ni Mungu, itakuwa Mungu watatu****; kwa kuwa mara tatu mmoja sio mmoja, bali watatu.* Kuna njia ambayo ni wamoja, lakini sio mtu mmoja, kama inavyo daiwa na Wanautatu.

*2. Kinyume na maandiko*. Karibu sehemu yoyote ya Agano Jipya ambayo tunaweza fungua mara nyingi inazungumza kuhusu Baba na Mwana, ina wawasilisha kama watu wawili tofauti. *Sura ya saba ya Yohana pekee inatosha kukanusha fundisho la Utatu.* Zaidi ya mara arobaini katika sura hiyo moja Kristo anazungumza kuhusu Baba yake kama mtu tofauti kutoka kwake mwenyewe. Baba yake alikuwa mbinguni naye duniani. Baba alikuwa *amemtuma. Amempa* ambao waliamini. Pia alikuwa *aende* kwa Baba. Na katika ushuhuda huu anatuonyesha ni katika nini kuna umoja wa Baba na Mwana. Ni umoja sawa na washiriki wa kanisa. “1li wawe na umoja kama vile Wewe Baba ulivyo ndani Yangu na Mimi nilivyo ndani Yako, wao nao wawe ndani yetu, ili ulimwengu upate kuamini ya kuwa Wewe ndiye uliyenituma Mimi. Utukufu ule ulionipa nimewapa wao, ili wawe na umoja kama Sisi tulivyo wamoja.” Wa moyo mmoja na nia moja. Wa lengo moja katika mpango wote uliowekwa kwa ukombozi wa mwanadamu. *Soma sura ya kumi na saba ya Yohana, uone kama haiondoi kabisa fundisho la Utatu*.

*Kuamini fundisho hilo, tunaposoma maandiko lazima tuamini kwamba Mungu alijituma ulimwenguni, akafa ili kuunganisha ulimwengu kwake, akajifufua*

*kutoka kwa wafu, akapaa kwake mwenyewe mbinguni, anatuombea kwake mwenyewe mbinguni, na ndiye mpatanishi kati ya wanadamu na yeye mwenyewe.* Haitafanya kubadilisha hali ya ubinadamu ya Kristo (kulingana na Utatu) kama Mpatanishi; kwa kuwa Clarke anasema, "Damu ya mwanadamu ya mwanadamu kamwe haiwezi mpendeza Mungu zaidi kuliko damu ya Nguruwe." Maoni. Juu ya 2Sam.xxi,10. *Pia lazima tuamini kwamba katika bustani Mungu alijiomba mwenyewe, ikiwa yawezekana, wacha kikombe hiki kiniondokee,* ***na upotovu mwingine elfu kama huo****.*

Soma kwa makini mafungu yafuatayo, ukiyalinganisha na dhana kwamba Kristo yuko kila mahali, jalali, mkubwa, na Mungu mwenye uwepo wake mwenyewe: Yohana xiv,28; xvii,3; iii,16; v,19,26; xi,15; xx,19; viii,50; vi,38; Marko xiii,32; Luke vi,12; xxii,69; xxiv,29; Matt.iii,17; xxvii,46; Gal.iii,20; 1Yno.ii,1; Ufu.v,7; Matendo xvii,31. Pia tazama Matt.xi,25,27; Luka i,32; xxii,42; Yohana iii,35,36; v,19,21,22,23,25,26; vi,40; viii,35,36; xiv,13; 1Kor.xv,28, &c.

*Neno utatu halipatikani popote katika Maandiko*. Fungu ambalo linafaa kufunza ni 1Yohana [5]:7, ambalo ni tafsiri. Clarke anasema, "katika miswada mia na kumi na tatu, fungu linadosari katika mia na kumi na mbili. Linatokea bila MS. Kabla ya karne ya kumi. Na mahali pa kwanza kutokea ni Uyunani, ni katika tafsiri za uyunani za matendo ya baraza la Lateran, lililofanyika A. D. 1215." - Som. juu ya Yohana i, na maoni mwisho wa sura.

*3. Asili yake ni ya kipagani na uwongo*. *Badala ya kutuelekeza kwa maandiko kwa uthibitisho wa utatu, tunaelekezwa kwa* Visa *(*trident) *vya Kiajemi, kwa madai kwamba "kwa hili ziliwekwa kufundisha dhana ya utatu, na kama walikuwa na fundisho la utatu, walikuwa wamelipokea kwa utamaduni kutoka kwa watu wa Mungu.* ***Lakini hayo yote yanadhahaniwa tu, kwa sababu ni kweli kwamba kanisa la Kiyahudi halikushikilia fundisho kama hilo****.* Bw. Summerbell anasema, **"rafiki yangu ambaye alikuweko katika Sinagogi ya *New York, alimuuliza Rabbi maelezo ya neno 'elohim'. Muhubiri wa Utatu aliyekuwa amesimama karibu, alijibu, 'mbona, hilo linarejelea watu watatu katika Utatu,' wakati Myahudi alisonga mbele na kusema asilitaje hilo neno tena, au watamlazimisha aondoke; kwa sababu haikuwa imeruhusiwa kutaja jina la mungu yeyote wa kigeni katika sinagogi*.**" (Majadiliano kati ya Summerbell na Flood

kuhusu Utatu, uk. 38) Milman anasema kwamba wazo la Trident ni uwongo. (Hist. Christianity, uk.34)

***Fundisho la Utatu lililetwa kanisani karibu wakati mmoja na ibada ya sanamu, na kuitunza siku ya jua, na ni fundisho la Waajemi tu likiteuliwa tena.*** *Lilishikilia karibu miaka mia tatu tangu kuanzishwa kwake kuleta fundisho kwa kile liliko sasa. Lilianzishwa kama 325 A. D., na halikukamiliki hadi 681*. Tazama Milman's Gibbon's Rome, vol. iv, uk.422. Lilipopokelewa Uhispania 589, Uingereza 596, Afrika 534. - Gib. vol. iv, uk.114,345; Milner, vol. i, uk.519." {J. N. Loughborough, *Review & Herald*, Novemba 5, 1861}

"Roho wa Mungu anazungumziwa katika Maandiko kama mwakilishi wa Mungu- uwezo ambao anatumia kutenda kazi, wakala ambaye vitu vyote vinashikamana. Hili lilionyeshwa wazi na waandishi wa Zaburi...Zab. 139:7-10. *Tunajifunza kutoka kwa lugha hii kwamba tunapozungumza kuhusu Roho wa Mungu kwa kweli tunazungumza kuhusu uwepo na uwezo wake*." {J. N. Loughborough, *Review & Herald*, Septemba 20, 1898}

"Zaidi ya hayo, yeye [kristo] ni mwanzo wa uumbaji wa Mungu. … ***Lugha kimsingi haiashiri kwamba aliumbwa***; kwa kuwa maneno… yanaweza tu onyesha kwamba kazi ya uumbaji, ikinena madhubuti, ilianzishwa naye. Bila yeye hakikuumbwa chochote. Wengine, hata hivyo, na kwa usahihi zaidi tunafikiria, wanachukua neno (la mwanzo kwa Kiyunani) kumaanishi wakala au ufanisi sababishi … kufahamu kwamba Kristo ndiye wakala ambaye kwake Mungu ameumba vitu vyote, *lakini yeye alikuja kuwepo kwa njia tofauti, kama anavyoitwa* ***mzaliwa pekee wa Baba***." {J. N. Loughborough, Insert A-1, *Lest We Forget*, Volume 4, Number 2, Second Quarter, 1994}

## Uriah Smith

(1832 – 1903)

"***Hakuna popote Maandiko yalizungumza kuhusu Kristo kama kiumbe wa kuumbwa, lakini kinyume inaelezea wazi kwamba alizaliwa na Baba.*** (Tazama maoni ya Ufu. 3:14, ***ambapo inaonyesha kwamba Kristo sio kiumbe wa kuumbwa***.) lakini kama Mwana hana umilele sawa wa awali kama Baba, *mwanzo wa uwepo wake,* ***kama mzaliwa wa Baba****, unatangulia kazi ya uumbaji, kwa kuhusiana kwamba anasimama kama muumbaji*

*mwenza na Baba.* Yohana 1:3; Ebr 1:2. Baba hangeteua kwamba kiumbe kama huyu aabudiwe sawasawa naye, bila hilo ni uabudu wa sanamu kwa upande wa mwabudu? Amemuinua katika nafasi ambayo inafanya sahihi kumuabudu, *na hata ameamuru kwamba aabudiwe, ambalo halingefaa kama angekuwa sawa na Baba katika umilele wa uwepo. Kristo mwenyewe alitangaza kwamba 'Kama vile Baba alivyo na uzima ndani Yake, vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na uzima ndani Yake.'* Yohana 5:26. Kwa hiyo Baba 'alimtukuza sana na kumpa Jina lililo kuu kuliko kila jina.' Flp. 2:9. Na Baba mwenyewe anasema, 'Malaika wote wa Mungu na wamsujudu.' Ebr. 1:6. Ushahidi huu wote unaonyesha kwamba Kristo anafaa kuabudiwa sawasawa na Baba; *lakini haudhibitishi kwamba pamoja naye anashikilia umilele wa uwepo uliopita.*" {U. Smith, *Thoughts on the Book of Daniel and the Revelation*, uk. 430. 1882}

***"Mungu pekee hana Mwanzo. Katika kipindi cha awali ambapo mwanzo unaweza kuwa, - Neno alitokea.*** "Hapo mwanzo, alikuwako Neno. Huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu." Yohana 1:1. ***Neno huyu ambaye hakuumbwa*** Alikuwako, ambaye, katika utimilifu wa wakati, alifanyika mwili, na akakaa miongoni mwetu. *Mwanzo wake haukuwa kama wa kiumbe mwingine yeyote ulimwenguni. Imewekwa kwa usemi wa ajabu, "mzaliwa wake [Mungu] wa pekee"* (Yohana 3:16; 1 Yohana 4:9), "Mwana wa pekee wa Baba" (Yohana 1:14), na, "nalikuja kutoka kwa Baba." Yohana 8:42. *Kwa hivyo inaonekana kwamba kwa msukumo au mchakato fulani mtakatifu, sio uumbaji, unaojulikana tu kuwa utu wa kufahamu yote, na pengine tu kwa mwenye uweza, Mwana wa wa Mungu alitokelezea. Na kisha Roho Mtakatifu* (kwa udhaifu wa tafsiri uitwao "the Holy Ghost"), ***Roho wa Mungu, Roho wa Kristo, msukumo takatifu na njia ya uwezo wao***, mwakilishi wa wote wawili (Zab. 139:7), pia alikuweko." {U. Smith, *Looking Unto Jesus*, uk. 10. 1898}

"1. Tunabatizwa kwa jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Matt. 28:19. Kwa hili tunaonyesha imani yetu kwa uwepo wa *Mungu mmoja wa kweli, upatanisho wa Mwanawe, na athari za Roho Mtakatifu*." {U. Smith, *The Bible Students Assistant*, uk. 21, 22. 1858}

"J. W. W. Anaauliza: "*Tunapaswa kuelewa kwamba Roho Mtakatifu (Holy Ghost) ni mtu*, kama walivyo Baba na Mwana? Wengini hudai ndivyo alivyo na wengine sivyo."

Jibu. – Istilahi “Holy Ghost”, ni tafsiri ngumu na asi. Inapaswa kuwa “Holy Spirit” (hagion pneuma) wakati. *Roho (Spirit) huyu wa Mungu, na Roho wa Kristo; Roho akiwa sawa kama anazungumziwa kuhusiana na Mungu au Kristo.* ***Lakini kuhusiana na Roho huyu, Bibilia inatumia kauli ambazo haziwezi kuwa na uwiano na wazo kwamba ni mtu kama walivyo Baba na Mwana***. *Badala yake inaonyeshwa kuwa athari takatifu kutoka kwa wote wawili, njia ambayo huwakilisha uwepo wao na ambayo kwayo wanaufahamu na uwezo katika ulimwengu wote, wakati ambapo hawako wenyewe.* Kristo ni mtu, sasa akihudumu kama kuhani katika Patakatifu pa mbinguni; na bado anasema wanapokusanyika pamoja watu wawili au watatu kwa jina langu, mimi niko papo hapo pamoja nao. Mt. 18:20. *Kwa njia gani? Sio yeye binafsi, bali kwa Roho wake. Katika mjadala mmoja wa Kristo (Yohana 14-16)* ***Roho huyu anahuishwa kama “Msaidizi,” na kwa hivyo yuko na utu na viwakilishi husika, “yeye,” “naye,” na “ndiye,” vikitumiwa kwake. Lakini anazungumziwa kwa njia ya kuonyesha kwamba hawezi kuwa mtu, kama Baba na Mwana***. *Kwa mfano, mara nyingi anasemwa “kumwagwa” na “kushushwa.” Lakini kamwe hatusomi kuhusu Mungu au Kristo kumwagwa au kushushwa. Kama angekuwa mtu, halingekuwa jambo geni kwake kuonekana kwa umbo la mwili; na bado wakati ambao ameonekana, ukweli huo umeonekana kuwa wa pekee.* Kwa hivyo Luka 3:22 inasema: “Roho Mtakatifu akashuka juu Yake kwa umbo kama la hua.” Lakini umbo haliwi sawa wakati wote; kwa sababu siku ya Pentekosti alichukua umbo la “ndimi za moto.” Matendo 2:3, 4. Tena tunasoma kuhusu “Roho saba wa Mungu wakitumwa katika ulimwengu wote.” Ufu. 1:4; 3:1; 4:5; 5:6. Hili ni wajibu wa Roho Mtakatifu usiotiliwa shaka, ukiwekwa katika umbo hili kuonyesha ukamilifu na utimilifu wake. *Lakini ingekuwa vigumu kuelezewa hivyo kama angekuwa mtu*. Hatusomi kuhusu Mungu saba au Kristo saba.” {U. Smith, *Review & Herald*, October 28, 1890}

“Hatutakuwa tumepotoka basi kuzingatia kwa muda huyu Roho ni nini, afisi yake ni gani, nini uhusiano wake kwa ulimwengu na kwa kanisa, na nini Mungu kupitia hili anapendekeza kufanya kwa watu wake. ***Roho Mtakatifu ni Roho wa Mungu; pia ni Roho wa Kristo. Ni uwepo huo mtakatifu, wa ajabu ambao kwao wanatenda kazi yao kuu na isiyo na mwisho.*** *... utagundua katika mafungu haya machache mtume analeta katika mtazamo*

*mashirika tatu makuu ambayo yanahusika katika kazi hii:* ***Mungu, Baba; Kristo, Mwanawe; na Roho Mtakatifu***." {U. Smith, *General Conference Daily Bulletin Volume 4*, March 14, 1891, uk. 146, 147}

## Stephen Nelson Haskell

(1833 – 1922)

"Wakati ulipopita katika mwaka wa 1844, hakukuwa na yeyote aliye amini ukweli kama tunavyoshikilia sasa. Wote waliamini unabii ambao ulitufikisha kwa wakati huo. Kisha wakaanza utafiti mkuu wa Bibilia kuliko ilivyokuwa awali, labda, wakati wowote tangu wakati wa mitume. Waliendelea zaidi na zaidi na majadiliano kuhusu unabii ambao uliwaelekeza kwa mwaka wa 1844, na baada ya uchunguzi wa kina hawakuona hitimisho nyingine kuliko kuwa unabii uliishia katika wakati huo. Walipokuwa wakisoma, walianza kuona kiungo kimoja cha ukweli baada ya kingine; na ukweli huu ulipokuwa ukijifunua kwa waanzilishi, -- Niko na urejeleo kwa watu kama hao Mzee James White, J. N. Andrews, Uriah Smith, na J. H. Wagoner, -- *hawakujaribu kuwasilisha ukweli huo kwa watu hadi walipoufanya suala la kipekee la maombi* ***na Roho wa unabii alikuwa ameweka muhuri wake juu yalo***." {S. N. Haskell, *Review and Herald*, Octoba 27, 1904}

"Upinde wa mvua katika mawingu ni mfano tu wa upinde ammbao umezunguka enzi tangu milele. *Nyuma katika kipindi, ambacho akili zenye mwisho haziwezi fahamu,* ***Baba na Mwana walikuwa peke yao ulimwenguni. Kristo alikuwa mzaliwa wa kwanza wa Baba, na Jehova alimjuza mpangilio takatifu wa Ukombozi***. Mpango wa uumbaji wa ulimwengu haukuwa umefunuliwa, pamoja na mpangilio wa viumbe ambavyo vitakuwa watu wao. Malaika, kama wawakilishi wa mpangilio mmoja, watakuwa wahudumu wa Mungu wa ulimwengu. Uumbaji wa ulimwengu wetu mdogo ulijumuishwa katika mipangilio ya kina iliyowekwa. Anguko la Lusifa lilionekana awali; vivyo hivyo uwezekano wa kuanzishwa kwa dhambi, ambayo ingeharibu ukamilifu wa kazi takatifu. *Hivyo basi ni katika siku hizo za awali, katika baraza hizo za awali, ndipo moyo wa Kristo uliguzwa;* ***na Mwana wa pekee*** *aliahidi kukomboa mwanadamu, iwapo atasikiliza na kuanguka.* ***Baba*** *na* ***Mwanao,*** *wakizungukwa na utakatifu uliofungamana, walishikana mikono.* … na ahadi ya milele ilitolewa; na *tangu hapo kuendelea* ***Baba na Mwana, kwa nia***

***moja**, walifanya kazi pamoja kukamilisha kazi ya uumbaji*. Kujikana nafsi kwa manufaa ya wengine kulikuwa msingi wa vyote.**"** {S. N. Haskell, *The Story of the Seer of Patmos*, uk. 93, 94. 1905}

**"**Kabla ya uumbaji wa ulimwengu wetu, "kulikuwa na vita mbinguni." ***Kristo na Baba waliahidiana pamoja; na Lusifa, Kerubi afunikaye, alijawa na wivu kwa sababu hakukubaliwa katika baraza la milele la Wawili walio kaa juu ya enzi**.**"** {S. N. Haskell, *The Story of the Seer of Patmos*, uk. 217. 1905}

**"*Kristo alikuwa mzaliwa wa kwanza mbinguni****;* vile vile alikuwa mzaliwa wa kwanza wa Mungu juu ya dunia, na mrithi wa enzi ya Baba. *Kristo, mzaliwa wa kwanza, ingawa Mwana wa Mungu*, alivikwa ubinadamu, na alifanywa mkamilifu kupitia kwa kuteseka. Alichukua namna ya mwanadamu, na milele yote, atasalia mwanadamu.**"** {S. N. Haskell, *The Story of the Seer of Patmos*, uk. 98, 99. 1905}

## George Ide Butler

(1834-1918)

**"**Mungu hukaa ndani yetu kwa Roho Mtakatifu, kama Msaidizi, kama Mwonyaji, hasa wa awali. Tunapokuja kwake tunashiriki naye kwa namna hiyo, *kwa sababu Roho hutoka kwake; hutoka kwa Baba na Mwana. Sio mtu akitembea kote* – pengine, kama sio, yuko zaidi kabisa ya ufahamu wangu wa maana ya lugha au maneno." **"** {Letter: G. I. Butler to J. H. Kellogg. April 5, 1904.}

## John Gottlieb Matteson

(1835-1896)

**"Kristo ndiye Mwana halisi wa Mungu**. "Mwana **Pekee** wa Baba." Yohana 1:14. Ni Mungu kwa sababu yeye ni Mwana wa Mungu; sio kwa ajili ya kufufuka kwake. Kama Kristo ndiye Mwana pekee wa Baba, basi hatuwezi kuwa wazaliwa wa Baba katika maana halisi. Inaweza kuwa tu katika maana ya pili ya ulimwengu.**"** {J. G. Matteson, Review & Herald, October 12, 1869 p. 123)

## Sarepta Myrenda (Irish) Henry

(1839 – 1900)

**"**"S. Unafikiria Roho wa Mungu ni mtu, au ni nguvu tu ambayo Mungu hutenda kazi, na ambayo amempa mwanadamu kwa matumizi yake?" "**J. viwakilishi vinavyotumika kuhusiana na Roho lazima vituelekeze kuhitimisha kwamba ni mtu, utu wa Mungu ambao ni chanzo cha uwezo wote na uzima**."**"** {S. M. Henry, The Abiding Spirit, 1899.}

## Dudley Marvin Canright

(1840 – 1919)

"'Kwa maana Mungu aliupenda ulimwengu akamtoa Mwanawe wa pekee,' &c. ***kulingana na hili, Yesu Kristo amezaliwa na Mungu kwa namna ambayo hakuna kiumbe kingine; vinginevyo hangekuwa Mwanawe wa pekee***. Malaika wanaitwa wana wa Mungu, na kwa hivyo ni watu watakatifu; *lakini Kristo ni Mwanawe kwa namna kuu, kwa uhusiano wa karibu, kuliko yeyote wa hawa*. Mungu aliumba watu na malaika kutoka kwa vitu ambavyo tayari vilikuwa vimeumbwa. Yeye ni mwanzilishi wa uwepo wao, muumbaji wao, na kwa hivyo Baba yao. ***Lakini Yesu Kristo alizaliwa kwa kiini cha Baba mwenyewe. Hakuumbwa*** *kutokana na vitu kama malaika na viumbe wengine walivyo.* Yeye ni kwa kweli na kwa msisitizo 'Mwana wa Mungu,'...Ebr.1:1-8 imenukuliwa. Kwa hili tunaona kwamba tofauti wazi na kuu inawekwa kati ya Mwana na malaika wote. Wote wanaamriwa kumwabudu. *Hakuna kiumbe aliyeumbwa anastahili kuabudiwa, licha ya ukuu anaoweza kuwa nao*, wala haitakuwa sahihi au haki kwa Mungu kutoa amri kwa mpangilio wa viumbe vyake kuabudu mwingine. Uungu pekee unastahili kuabudiwa, na kuabudu kingine chochote itakuwa ibada ya sanamu. Kwa hivyo Paulo anamweka Kristo juu zaidi kuliko malaika, na anafanya tofauti kubwa kati yao." {D. M. Canright, *Review & Herald*, June 18, 1867}

"Katika wakati ambao Bibilia iliandikwa, karibu ulimwengu wote ulikuwa umepokea miungu wengi au imani ya miungu. *Imani hii ilifundisha kwamba kulikuwa na miungu wengi*. Roma ilikuwa na miungu yake. Uyunani walikuwa na miungu yao. Misri walikuwa na miungu yao. ... *kwa upinzani wa hilo. Musa na manabii waliweka ukweli mkuu kwamba* ***fundisho hili la***

***miungu wengi lilikuwa uwongo, na kwamba kulikuwa Mungu mmoja tu...*** "'Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.' Kumb. 6:4. ***Hapa tunapiga hoja muhimu ya fundisho la Mungu. 'Sikiza, Ee Israeli; Bwana, Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja.' Sio wengi, sio elfu, sio mia, sio kumi, sio watatu, ila tu MMOJA Mungu mmoja.*** *... Tukigeukia Agano Jipya, tunapata fundisho sawa wazi kama tu katika Agano la Kale. Musa wala manabii hawakuweka umoja wa Mungu dhabiti zaidi kuliko Yesu mwenyewe.* Aliufundisha na akarudia mara nyingi. Kwa hivyo anasema: 'Amri iliyo kuu ndiyo hii, Sikiza Ee Israeli, Bwana Mungu wetu, Bwana ndiye mmoja. Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, kwa roho yako yote, kwa akili zako zote na kwa nguvu zako zote. Ya pili ndiyo hii: 'Mpende jirani yako kama nafsi yako. Hakuna amri nyingine iliyo kuu kuliko hizi. Yule mwalimu wa sheria akamwambia Yesu, Mwalimu, umejibu vema kwamba Mungu ni mmoja wala hakuna mwingine ila Yeye.' Marko 12:29-32. "Waandishi walisema, 'Kuna Mungu mmoja, na hakuna mwingine ila yeye.' Kwa tamko hili Yesu alitoa kibali. 'Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma.' Yohana 17:3 ***Yesu anasema kuwa Baba yake ndiye tu Mungu wa kweli wa pekee. Lakini wana-utatu wanatoa mawazo kinzani kwa kusema kwamba Mwana na Roho Mtakatifu ni Mungu wa kweli sawa tu na Baba alivyo... [1 Kor. 8:4-6 imenukuliwa] "Anasema mtume mkuu, 'Hakuna Mungu mwingine ila mmoja,' na 'Yuko Mungu mmoja, aliye Baba, ambaye vitu vyote vyatoka Kwake.' Anatwambia huyu Mungu mmoja ni nani. Sio Roho Mtakatifu, sio Yesu Kristo, ila ni Baba. Gal. 3:20; 1 Tim. 1:17… Jinsi ambavyo fundisho la Utatu, la Mungu wa tatu, linaweza shikamanishwa na kauli hizi sijui***. …

*Na wakati ambao Bibilia kamwe haitumii kirai, 'Utatu,' 'Mungu wa utatu,' 'watatu katika mmoja,' 'watu watakatifu,' Mungu Roho Mtakatifu,' n.k. lakini inasema kwa msisitizo kuna Mungu mmoja tu, Baba.* ***Na kila majadiliano kujaribu kuthibitisha Mungu watatu ndani ya mtu mmoja, Mungu Baba, Mungu Mwana, na Mungu Roho Mtakatifu, wote wa kiini sawa, na sawa kwa kila njia, na wote watatu wakiunda mmoja tu, inajipinga, inapingana na mantiki, na inapingana na Bibilia...*** "Mungu ana uwepo wake mwenyewe, na chanzo na mwanzilishi wa vitu vyote,-wa malaika, wa watu, wa ulimwengu wote,-wa kila kitu. Kwa hivyo Paulo

anasema, 'Kwa maana vitu vyote vyatoka Kwake, viko Kwake na kwa ajili Yake. Utukufu ni Wake milele. Amen.' Rum. 11:36. "Yeye ni chanzo cha uzima na umilele. Kwa hivyo, akizungumza kuhusu Baba, Paulo anasema, 'Yeye peke yake hapatikani na mauti, ambaye anakaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa.' 1 Tim. 6:16. Tambua kwamba Mungu huyu mtukufu ni yeye tu ambaye, hapatikani na mauti..." 'Kama vile Baba alivyo na uzima ndani Yake, vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na uzima ndani Yake.' Yohana 5:26. Kauli hii ina usahihi. *Baba ana uzima ndani yake, na katika upendo wake mkuu aliweka zawadi sawa juu yake; lakini itagunduliwa kwamba Baba mmoja ambaye zawadi ilitoka kwake...* ni jinsi gani Paulo anatofautisha Baba na Mwana kwa makini. Anasema, 'Baba, ambaye vitu vyote vyatoka kwake,' na 'Yesu Kristo, ambaye vitu vyote ni kwake.' *Baba ni chanzo cha kila kitu. Kristo ndiye ambaye vitu vyote vinaumbwa kwake. Mamlaka yote, utakatifu, na uwezo wa Kristo alipokea kutoka kwa Baba... Imani kwa fundisho hili ni muhimu sana. Kwa kweli, haiwezi ikasisitizwa kwa nguvu zaidi*. Yesu hata anatangaza kwamba ufahamu wa ukweli huu ni muhimu kwa uzima wa milele. 'Nao uzima wa milele ndio huu, wakujue Wewe uliye Mungu wa pekee, wa kweli na Yesu Kristo uliyemtuma.' Yohana 17:3. ***"Lazima tumjue Baba kama Mungu pekee wa kweli. Na hakuna Mungu wa kweli zaidi ya Baba. Lakini lazima pia tujue Mwanawe Yesu Kristo, ambaye alimtuma. Ni jinsi gani fundisho hili lilivyo rahisi na wazi, na ni kwa wingi namna gani limedumishwa na Roho Mtakatifu.***" {D. M. Canright, *Review & Herald*, August 29, 1878}

## Alonzo Trevier Jones

(1850-1923)

**"***Ambaye alizaliwa kwa umbo la Mungu akachukua umbo la mwanadamu*. "Katika mwili wakati huo wote alikuwa kama Mungu, lakini hakuonekana kama Mungu." "Alijitowa katika umbo la Mungu, na kwa niaba yake akachukua umbo na mtindo wa mwanadamu." "Utukufu wa umbo la Mungu, kwa muda alisimamisha."**"** {A. T. Jones, *G. C. Bulletin 1895*, p. 448}

**"**Alizaliwa kwa Roho Mtakatifu. Kwa njia nyingine, Yesu Kristo alizaliwa tena. *Alitoka mbinguni,* ***mzaliwa wa kwanza wa Mungu***, akaja duniani, *na akazaliwa tena*. Lakini yote katika kazi ya Kristo huenda kwa kinyume kwetu: Yeye, ambaye hakuwa na dhambi, alifanywa kuwa dhambi ili

kwamba tuhesabiwe haki kwa Mungu katika yeye. Yeye, anayeishi, Mfalme na Mwanzo wa uzima, alikufa ili tuishi. *Yeye ambaye kuzaliwa kwake kumekuwa tangu siku za milele,* ***mzaliwa wa kwanza wa Mungu***, alizaliwa tena ili tuweze kuzaliwa tena.**”** {*Christian Perfection*, pr. 53. A Sermon by A. T. Jones, *Review & Herald*, July 18-August 1, 1899}

## Hampton Watson Cottrell

(1852 – 1940)

**“**Hitimisho iliyofikiwa wakati huo [wakati wa waanzilishi] ilikuwa kwamba *Roho Mtakatifu hakuwa mtu kwa namna ambayo Mungu na Kristo ni watu,* kama ndivyo, ugumu sawa unaweza shuhudiwa na Roho Mtakatifu kuwa kila mahali kama inavyoshikiliwa na Wana-utatu kuhusiana na Mungu na Kristo kama watu wakiwa kila mahali, na kama itakubalika *Kristo atakuwa Mwana wa Roho Mtakatifu, badala ya Mwana wa Baba kama Bibilia inavyomtangaza kuwa*.**”** {Letter of H. W. Cottrell to LeRoy Froom, September 16, 1931}

## James Edson White

(1849 – 1928)

**“**Malaika, kwa hivyo, ni viumbe wa kuumbwa, kimsingi wa cheo cha chini kidogo kuliko Muumbaji wao. ***Kristo ndiye kiumbe pekee mzaliwa wa Baba***.**”** {J. E. White, *Past, Present and Future*, uk. 52. 1909}

**“*****Kiumbe mmoja tu ulimwenguni kando na Baba ana jina la Mungu, na huyo ni Mwanawe, Yesu Kristo***.**”** {J. E. White, *The Coming King*, uk. 33}.

## William Clarence White

(1854 – 1937)

**“**Katika barua yako unaniomba kuelezea kile ambacho ninafahamu kuwa katika msimamo wa mama yangu kuhusiana na utu wa Roho Mtakatifu. Hili siwezi fanya kwa sababu sikuelewa vyema fundisho lake kuhusiana na suala hilo. Kila wakati kulikuwa na kuchanganyikiwa fulani katika mawazo yangu kuhusiana na kutamka kwake ambako kwa jinsi yangu ya kuwaza kwa juu juu kulionekana kukanganya kiasi. Mara nyingi nimejuta kwamba sikuwa na makini hiyo ya mawazo ambayo ingesuluhisha hili na kuchanganyikiwa sawa, na kisha kukumbuka kile ambacho Dada white aliandika katika

‘*Matendo ya Mitume*,’ Ukurasa 51 na 52, ‘kuhusiana na siri kama hizo ambazo ni za kina zaidi kwa ufahamu wa mwanadamu, kimya ni dhahabu,’ nimeona vyema kujiepusha na majadiliano na kujitahidi kuelekeza mawazo yangu kwa masuala ambayo ni rahisi kuelewa.

Ninaposoma Bibilia, ninapata kwamba Mkombozi aliyefufuka alipulizia wanafunzi ‘na kuwaambia, pokeeni Roho Mtakatifu.’ Dhana ambayo inapokelewa kutoka kwa Fungu hili, inaonekana kuwa na uiano na kauli katika ‘*Desire of Ages’*, ukurasa 669, pia Mwanz. 1:2; na Luka 1:4; na Matendo 2:4 na pia 8:15 na 10:44. Mafungu mengine mengi yanaweza rejelewa ambayo yanaonekana kuwa na uiano na kauli hii katika ‘*Desire of Ages.*’ ***Kauli na hoja za baadhi ya wahudumu wetu, katika jitihada zao kuthibitisha kwamba Roho Mtakatifu ni mtu binafsi kama walivyo Mungu Baba na Kristo, Mwana wa milele, zimenichanganya, na wakati mwingine, zimenihuzunisha. Mwalimu mmoja maarufu alisema ‘Tunaweza mchukulia, kama mshirika ambaye yuko hapa chini akiendesha mambo.’*** Kuchanganyikiwa kwangu kulipunguzwa kidogo nilipojifunza kutoka kwa kamsi kwamba moja ya maana ya utu, ilikuwa tabia. ***Ilieleza kwa njia ambayo nilihitimisha kwamba kunaweza kuwa na utu bila umbo la mwili ambalo liko na Baba na Mwana.*** *Kuna mafungu mengi ambayo yanazungumza kuhusu Baba na Mwana na ukosefu wa Andiko likifanya marejeleo sawa kwa kazi moja ya Baba na Roho Mtakatifu au ya Kristo na Roho Mtakatifu,* ***imeniongoza kuamini kwamba roho bila utu binafsi alikuwa mwakilishi wa Baba na Mwana katika ulimwengu wote, na nikupitia kwa Roho Mtakatifu wanaishi ndani ya mioyo yetu na kutufanya wamoja na Baba na Mwana*.”** {Barua, W. C. White kwa H. W. Carr, Aprili 30, 1935}

## Milton Charles Wilcox

(1853 – 1935)

**“**Mungu ni chanzo cha uzima...uzima wa Mungu ni wa milele, kama alivyo ‘Mungu wa Milele.’*...’lakini Mungu ni mtu; uzima wake unawezaje kuwa kila mahali?’ Mungu yuko kila mahali kwa Roho wake...****uwepo wa Mungu kwa hivyo ni Roho Mtakatifu; na Roho Mtakatifu kwa hivyo ni uzima wa Mungu***. Na hivyo tunasoma kuhusu ‘Roho wa Uzima’ (Rum. 8:2), kwamba ‘Roho yuko hai kwa sababu ya haki’ ([f.] 10); kwamba ‘Roho hutoa uzima’

(2 kor. 3:6).**"** {M. C. Wilcox, *Signs of the Times*, June 2, 1898}

**"**Swali 187: *Ni nini tofauti kati ya Roho Mtakatifu na roho zinazohudumu (malaika), au wako sawa?*

Jibu: *Roho Mtakatifu ni nguvu yenye uwezo ya Uungu (Godhead), uzima na uwezo wa Mungu ukitiririka kutoka kwake kwa sehemu zote za ulimwengu, na kwa hivyo akifanya muunganiko wa uzima kati ya enzi yake na uumbaji wote.* Kama inavyoelezewa na mwingine: "Roho Mtakatifu ni pumzi ya uzima wa kiroho nafsini. ***Kuondoka kwa Roho ni kuondoka kwa uzima wa Kristo****." Kwa hivyo humfanya Kristo kuwa kila mahali*. Kutumia mfano ghafi, kama tu simu ibebavyo sauti ya mtu, na kuifanya kuwa mbali sana, *hivyo Roho Mtakatifu hubeba uwezo wote wa Kristo na kuufanya kuwa kila mahali kwa nguvu zake zote, na kumdhihirisha kwa wale wenye uiano na sheria yake.* ***Kwa hivyo Roho anahuishwa katika Kristo na Mungu, lakini haonyeshwe kama mtu tofauti****. Kamwe hatuambiwi kumuomba Roho; mbali Mungu kwa Roho. Kamwe hatupati katika Maandiko maombi kwa Roho, bali ya Roho.***"** {M. C. Wilcox, *Questions and Answers Gathered From the Question Corner Department of the Signs of the Times,* uk. 181, 182. 1911}

**"**Utukufu mkuu na usioweza kustahimilika wa Uungu (Godhead) unawakilishwa katika Baba. 1 Tim. 6:16. *Yesu Kristo daima amechanganya uungu na ubinadamu,* ***na kutoka kwake anatiririka Roho wa uzima kwa watoto wake wote.*** Malaika ni njia, nguzo, ambazo mikondo hii mikuu ya uzima wa Mungu inaimarika, hivyo ni kusema, mikondo ya uzima. Wanaweza kustahimili bila kuinuliwa Roho wa Mungu na utukufu wake mkuu, na ndani yao walete uwepo wa Mungu kwa wanawe, na kuwafukuzilia mbali malaika waovu ambao hutafuta kuwaangamiza.**"** {M. C. Wilcox, *Signs of the Times*, Feb. 26, 1908}

**"**28.UTU WA ROHO *Swali. 1. Baadhi husema Roho Mtakatifu ni mtu; wengine husema ni utu; na wengine, nguvu tu. Hadi lini hili litakuwa suala la majadiliano? Jibu. 1. Utu wa Roho Mtakatifu utakua suala la majadiliano daima. Wakati mwingine Roho anatajwa kama 'anamwagwa,' Kama katika Matendo 2. Kote katika Maandiko, Roho amewasilishwa kama nguvu ya Mungu itendayo kazi...****Sababu ambayo Maandiko yanazungumza kuhusu Roho kama mtu, inaonekana kwetu, kwamba inaleta kwetu, na kwa kila***

***roho iaminiyo, uwepo binafsi wa Bwana wetu Yesu Kristo***...

"Kwa sababu ya kukosa imani, 'ilifaa' lazima aondoke; kwa maana anasema, 'Lakini amin nawaambia, yafaa Mimi niondoke kwa kuwa nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu, lakini nikienda nitamtuma kwenu.' Yohana 16:7. Wanafunzi wake hawangetambua uwepo wa Roho mtakatifu kadri Kristo alivyokuwa nao binafsi. Kwa njia hiyo, angekuwa tu nao walikuwa karibu naye. *Lakini alipoondoka, na Roho akaja, angefanya Kristo kuwa na kila mmoja, popote huyo mmoja alikuwa na Paulo Athene, Petro Yerusalemu, Tomaso India, Yohana katika Patimo.*

*"Hii ni mifano tu. Popote wana wa Mungu walipo, kuna Roho –* ***sio mtu binafsi, kama tunavyo watazama watu, bali kuwa na nguvu za kumfanya Baba na Mwana kuwepo****. Roho huyo anawekwa katika wajumbe wa Mungu, malaika; lakini malaika sio Roho. Wanadumishwa na Roho, na kutumiwa na Roho, na wako na nguvu za Roho ndani yao; lakini wao sio Roho. Roho yuko huru kwa mashirika haya ya watu na vitu. Mbona tusiachie?* ***Mbona tusijue kwamba Roho, Roho wa Mungu, Roho wa Kristo, Roho wa Uungu, huenda kote ulimwenguni, akileta uwepo wa Mungu katika kila moyo unaompokea?"*** {M. C. Wilcox, *Questions And Answers Vol.11*, 1919. 1938 ed., uk.37-39. In 1945 ed. uk.33-35}

## Ellet J. Waggoner
(1855 – 1916)

"Neno alikuwako "hapo mwanzo." ***Mawazo ya mwanadamu hayawezi shika miaka ambayo inatajwa katika kirai hiki. Haijawekwa wazi kwa wanadamu kujua lini au jinsi Mwana alizaliwa;*** Lakini tunajua kwamba alikuwa Neno Takatifu, sio tu kabla ya kuja katika ulimwengu huu kufa, bali hata kabla ya ulimwengu kuumbwa. Kabla ya kusulubiwa kwake aliomba, "Hivyo sasa, Baba, unitukuze mbele Zako kwa ule utukufu niliokuwa nao pamoja na Wewe kabla ulimwengu haujakuwako." Yohana 17:5. Na zaidi ya miaka mia saba kabla ya kuja kwake mara ya kwanza, kuja kwake kulikuwa kumetabiriwa kwa neno la uvuvio: "Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele."

Mika 5:2, kiasi. ***Tunajua kwamba Kristo "alitoka kwa Mungu" (Yohana 8:42), lakini ilikuwa mbali zaidi katika miaka ya milele ambayo haiwezi eleweka na mawazo ya mwanadamu.*** {E. J. Waggoner, *Christ And His Righteousness*, p. 9. 1890}

**"Kristo ni Mungu?**

…*Kristo hakupewa jina hili kwa ajili ya athari ya mafanikio fulani*, ***bali ni haki yake ya urithi***. Tukizungumza kuhusu uwezo na ukuu, mwandishi wa Waebrania anasema kwamba Kwa hiyo alifanyika bora kuliko malaika kwa sababu, "amepokea Jina kwa urithi lililo bora kuliko lao." Ebr. 1:4. *Mwana wakati wote huchukua jina la baba;* ***na Kristo, kama "Mwana wa pekee wa Mungu," kwa haki yuko na jina sawa***. *Mwana pia kwa kiwango kikuu au kidogo, ni uzazi wa baba; kwa kiwango fulani yuko na vipengele na tabia za baba yake; sio kamili, kwa sababu hakuna uzazi kamili miongoni mwa wanadamu. Lakini hakuna kasoro kwa Mungu, au katika kazi yake yoyote, na kwa hivyo Kristo ni "mfano halisi" wa nafsi ya Baba. Ebr. 1:3****. Kama Mwana wa Mungu mwenye uwepo wake mwenyewe, yuko na kiasili tabia zote za Uungu.***

***Ni ukweli kwamba kuna wana wengi wa Mungu, lakini Kristo ndiye "mzaliwa wa pekee wa Mungu," na kwa hivyo Mwana wa Mungu kwa namna ambayo hakuna kiumbe mwingine alikuwa au anaweza kuwa***. *Malaika ni wana wa Mungu, kama alivyo kuwa Adamu (Ayubu 38:7; Luka 3:38), kwa uumbaji; Wakristo ni wana wa Mungu kwa kufanywa wana. (Rum. 8:14, 15****), lakini Kristo na Mwana wa Mungu kwa kuzaliwa***. Mwandishi kwa Waebrani anazidi kuonyesha kwamba cheo cha Mwana wa Mungu sio ambacho Kristo ameinuliwa kwacho, mbali hicho ndicho alicho nacho kwa *haki*." {E. J. Waggoner, *Christ And His Righteousness*, pp. 11-13. 1890}

"Neno la tahadhari linaweza kuwa muhimu hapa. *Mtu yeyote asidhani kwamba tutamuinua Kristo kwa hasara ya Baba au kumpuuza Baba*. Hilo haliwezekani, kwa kuwa azimio lao ni moja. Tunamheshimu Baba kwa kumheshimu Mwana. *Tunazingatia maneno ya Paulo, kwamba "*kwetu sisi yuko Mungu mmoja, aliye Baba, ambaye vitu vyote vyatoka Kwake na kwa ajili Yake sisi twaishi na kuna Bwana mmoja tu, Yesu Kristo, ambaye kwa Yeye vitu vyote vimekuwepo na kwa Yeye sisi tunaishi*" (1 Kor. 8:6);*

kama vile tayari tumenukuu, kwamba ni kwa yeye Mungu aliumba ulimwengu. Kwake utimilifu wote unakaa, na kwamba amekuwa halisi, na wakala aliyepo wa kila tendo la uumbaji. *Lengo letu katika utafiti huu ni* ***kuweka cheo cha Kristo cha haki*** *cha usawa na Baba, katika cheo kwamba uwezo wake wa kukomboa unaweza thaminiwa vyema*." {E. J. Waggoner, *Christ And His Righteousness*, Uk. 19. 1890}

**"Kristo ni Kiumbe wa Kuumbwa?**

*Kabla ya kuingia katika baadhi ya masomo halisi ambayo yatajifunzwa kutokana na ukweli huu, lazima tukae kwa muda mchache katika maoni ambayo yameshikiliwa kwa uaminifu na wengi ambao hawawezi kwa fikara yoyote ya hiari taka kutomtii Kristo, bali ambao,* ***kupitia kwa maoni hayo, kwa kweli hukataa Uungu wake****, ambaye, kupitia kwa radhi njema ya Mungu, aliinuliwa katika nafasi yake ya juu. Hakuna yeyote ambaye hushikilia mtazamo huu anaweza kuwa na msimamo wowote wa cheo cha haki cha juu ambacho Kristo kwa kweli anakaa.*

*…**Maandiko yalitangaza kwamba Kristo ni "Mwana wa Pekee wa Mungu." amezaliwa, sio kuumbwa. Kuhusu wakati ambao alizaliwa, sio kazi yetu kuuliza, wala mawazo yetu hayawezi shika kama tungeambiwa.**. Nabii Mika anatwambia kila kitu ambacho tunaweza jua kuhusu hilo katika maneno haya, "Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele." Mika 5:2, kiasi.* ***Kuna wakati ambao Kristo alitoka kwa Baba, kutoka kwa kifua cha Baba (Yohana 8:42; 1:18), lakini wakati huo ulikuwa mbali sana katika siku za umilele kwamba kwa ufahamu wenye mwisho hihalisia hauna mwanzo****.*

***Lakini hoja ni kwamba Kristo ni Mwana wa kuzaliwa na sio mada ya kuumbwa.*** *Ana jina bora kuliko malaika kwa urithi*; yeye ni "Mwana juu ya nyumba yake mwenyewe." Ebr. 1:4; 3:6. ***Na kwa vile ni Mwana wa pekee wa Mungu, ni wa kiini sawa hasa na asili ya Mungu na yuko na sifa zote za Baba kwa kuzaliwa, kwa kuwa Baba alipendezwa kwamba Mwanawe awe mfano wake wa moja kwa moja, mng'ao wa utukufu wake, akijawa na utimilifu wote wa Uungu****….*

***Hatimaye, tunajua umoja wa Uungu wa Baba na Mwana kutoka kwa ukweli kwamba wote wako na Roho sawa****. Paulo, baada ya kusema kwamba walio katika mwili hawawezi mpendeza Mungu, anaendelea: "Lakini ninyi, hamtawaliwi na mwili, bali na Roho, ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu. Mtu ye yote ambaye hana Roho wa Kristo, yeye si wa Kristo." Rum. 8:9.* ***Hapa tunapata kwamba Roho Mtakatifu ni Roho wa Mungu na pia Roho wa Kristo****.* Kristo "yuko katika kifua cha Baba" akiwa kiasili wa kiini hasa cha Mungu na kuwa na uzima ndani yake mwenyewe. Kwa usahihi anaitwa Yehova, mwenye uwepo wake na kwa hivyo anawekwa katika Yer. 23:5, 6, ambapo inasemwa kwamba Chipukizi la haki, ambaye atafanya hukumu na haki katika nchi, na jina lake atakaloitwa ni hili 'Jehovah-tsidekenu'—BWANA, HAKI YETU. *Mtu awaye yote, ambaye anamheshimu Kristo kwa vyote, asimpe heshima ndogo kuliko ile anayompa Baba, kwa kuwa hii itakua kukosa kumheshimu Mungu zaidi*, lakini wote, pamoja na malaika mbinguni, wamwabudu Mwana, bila hofu yoyote kwamba wanaabudu na kutumikia kiumbe badala ya Muumbaji." {E. J. Waggoner, *Christ And His Righteousness*, Uk. 19-24. 1890}

"*Katika kujadili usawa kamili wa Baba na Mwana, na ukweli kwamba Kristo katika kila hali ni Mungu,* ***hatubuni kueleweka kufundisha kwamba Baba hakuwepo kabla ya Mwana****.* Haitakuwa muhimu kuilinda hoja hii, au wengine watadhani kwamba Mwana alikuwepo wakati mmoja na Baba; ***ila baadhi wanaenda zaidi, jambo ambalo haliongezi chochote kwa heshima ya Kristo, lakini badala yake huondoa heshima ambayo amepewa****, kwa vile wengi hutupilia mbali suala lote badala ya kukubali nadharia wazi kabisa haina uiano na lugha ya Maandiko,* ***kwamba Yesu ni Mwana wa pekee wa Mungu. Alizaliwa, sio kuumbwa. Ni wa kiini cha Baba, hivyo kwamba kwa kila hali ni Mungu***; na kwa vile hili ndivyo 'Kwa kuwa ilimpendeza Mungu kwamba ukamilifu Wake wote wa kimungu uwe ndani Yake.' Kol. 1:19... ***kwa vile wote ni wa hali sawa, Baba ni wa kwanza kwa wakati. Pia ni mkuu kwa sababu hakuwa na mwanzo, wakati ambao utu wa Kristo ulikuwa na mwanzo***." {E. J. Waggoner, *Signs of the Times*, April 8, 1889}

| | |
|---|---|
| "Malaika ni wana wa Mungu, kama alivyokuwa Adamu…kwa kuumbwa; *Wakristo ni wana wa Mungu kwa kufanywa wana* (Rum. 8:14, 15), **lakini Kristo ni Mwana wa Mungu kwa kuzaliwa.** … na kwa hivyo Kristo ni "mfano halisi" wa nafsi ya Baba." {E. J. Waggoner, *Christ And His Righteousness*, p. 12. ***1890***} | "'Mungu aliupenda ulimwengu, akamtoa Mwanawe wa pekee,'—sio mwana kwa kuumbwa, kama walivyokuwa malaika, *wala mwana kwa kufanywa, kama alivyo mdhambi aliyesamehewa*, **bali Mwana mzaliwa katika mfano** halisi wa nafsi ya Baba…" {E. G. White, *Signs of the Times*, May 30, ***1895***} |

## William Warren Prescott

(1855–1944)

**"**Kama Kristo alivyozaliwa mara mbili, **mara moja katika umilele, Mwana wa pekee wa Baba**, na tena hapa katika mwili, kwa hivyo akiunganisha uungu na ubinadamu katika kuzaliwa kwa pili, ndivyo sisi, ambao tumezaliwa mara moja katika mwili, tutakuwa na kuzaliwa kwa pili, kuzaliwa upya kwa Roho, ili kwamba uzoefu wetu uwe sawa, ubinadamu na uungu ukiunganishwa katika unganiko la uzima.**"** {W. W. Prescott, Review & Herald, April 14, 1896, uk. 232}

## Judson Sylvaneous Washburn

(1863 – 1955)

"Fundisho la Utatu linachukuliwa kama jaribio kuu la Uorthodoxi na Kanisa Katoliki la Roma. Mengi ya mabaraza mengi ya kanisa hilo wakati lilikuwa likianzishwa walikuwa karibu wote wamekubaliana na majadiliano ya Utatu, Uariani, na utata wa Utatu.

"Kristo alikuwa wa kiini sawa na Baba, au wa kiini cha mfano?" kihalisia kabisa asili ya utu wa Mungu ilikuwa mada kuu, msingi, ufunguo wa mafundisho ya theolojia ya Rumi, kito cha dhamani cha Shetani cha Ukristo Potofu Bandia.

Mafundisho yanayoongoza ya Papa wa Rumi yalichukuliwa moja kwa moja kutoka kwa upagani (heathenism), -alama ya msalaba, maji Matakatifu, watawa, sista, useja wa maaskofu, Sabbato ya Jumapili, n.k. Kwa hivyo

Fundisho hili la Katoliki linatoka kwa upagani. India tuko na Brahma, Shive, Vishnu, utatu usio samehe, wa kulipiza kisasi.

Ni wapi katika Upagani au katika Urumi kuna Mpatanishi Mtakatifu kati ya Mungu na Mwanadamu? "Kwa maana kuna Mungu mmoja na mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, yaani, mwanadamu Kristo Yesu." I Tim. 2:5. Hakuna yeyote katika upagani; na katika Kanisa la Roma, kama Kristo alivyo sehemu halisi ya Mungu, uungu, inakuwa muhimu kuzua wapatanishi wengi wa kibinadamu, bikira Maria, Petro, Andrea, n.k. na watakatifu wengi wa kujitengenezea, kundi la mioyo isiyokufa ya waume na wake waliokufa. Yesu amekuwa kikamilifu na kihalisia sehemu ya kipengele cha hukumu hiyo kali na kuu ambaye anafurahia kwa mateso ya milele, kulinga na mafundisho ya Roma ya Utatu, kwa lazima watafute au watengeneze kundi la wanadamu wapatanishi wa kiroho. HUKU KUMUONDOA YESU KATIKA UHUSIANO WAKE WA KWELI NA MUNGU NA MWANADAMU, HUMCHUKUA MBALI ZAIDI NASI KWAMBA ANAKUWA MPOKEAJI WA MATESO YA MILELE NA KAMWE SIO MKOMBOZI WETU MWENYE UPENDO.

Fundisho la Utatu ni mnyama katili wa kipagani, likimwondoa Yesu katika cheo chake cha kweli cha Mkombozi Mtakatifu na Mpatanishi. Ni ukweli hatuwezi pima au kuelezea uungu. Ni zaidi ya ufahamu wetu, ila katika mada hii ya utu wa Mungu Bibilia inaelezea virahisi na wazi. **Baba, Mzee wa Siku, ni tangu milele. Yesu alizaliwa na Baba. Yesu akizungumza kupitia kwa Wana-Zaburi anasema**:

Nitaihubiri amri; Bwana (Yehova) aliniambia, Ndiwe mwanangu, Mimi leo nimekuzaa. Zaburi 2:7.

Tena katika Methali nane (ambapo Kristo anazungumziwa chini ya jina Hemima, Tazama I Wakorintho 1:24), tunasoma: Bwana (Yehova) alinimiliki katika mwanzo wa njia yake. Fungu 22. Kabla ya milima kuumbwa, kabla ya vilima nalizaliwa. Fungu 24.

Mwana anasema kwamba alitoka, alizaliwa na Baba yake (Yehova). Anamuita Baba yake "Yehova." Katika Zaburi 110:1, Bwana alimwambia Bwana wangu, keti katika mkono wangu wa kuume, n.k. Kiebrania Halisi, "Yehova alimwambia Adoni," Yehova (Baba) alimwambia Adoni (mwana).

Psalm 110:4, Bwana (Yehova) ameapa na hatabadilika, Wewe ndiye kuhani milele, kwa mfano wa Melkizedeki. Kuhani huyu mfano wa Melkizedeki ni nani? Ni Yesu. Tazama Waebrania 7:21, 22; Marko 19:35, 36.

Katika maandiko haya Yesu mwenyewe anasema jina la Baba ni Yehova, jina lake mwenyewe Adoni. Ikiwekwa katika Kutoka 23:31, Bwana alisema atatuma Malaika wake mbele ya watu wake, kihalisia Mjumbe wake, na akasema, "Jina langu liko katika Yeye," kwa hivyo Mungu aliweka jina lake kwa Mwanawe. Na hivyo duniani jina la kila baba liko kwa mwanawe. Kwa hivyo ni halali kusema kwamba Mwana anaweza zungumziwa kama Yehova, ikiwekwa kimsingi, Mwana alisema jina la Baba yake ni Yehova...

Shetani amechukua baadhi ya mawazo ya mataifa ya kiumbe wa kuchusha mno mwenye vichwa saba, na kwa mwelekeo makusudi wa kuweka dharau kwa uungu, ameyavuma katika Urumi kama Mungu wetu mtakatifu, uvumbuzi usio wezekana, na usio mantiki. Fundisho likipandikizwa kutoka kwa mataifa hadi kwa Kanisa la Kipapa la Roma linajaribu kuingiza uwepo wake muovu katika mafundisho ya Ujumbe wa Malaika wa Tatu...

Utu tofauti wa Baba na Mwana ni muhimu sana kwa mpango wa wokovu. Ilikuwa muhimu, muhimu kabisa kwamba Kristo alipokuwa amekufa, Baba aishi na kuendelea kushikamanisha vitu vyote na kumuondoa Yesu kwenye kaburi. Kristo ni yeye, mpatanishi pekee kati ya Mungu, Baba na mwanadamu. Kama Baba na Mwana ni "mtu mmoja," basi Kristo ni mpatanishi kati yake yeye mwenyewe na Mwanadamu. Kristo alifanywa kwa mfano halisi wa nafsi ya Baba. Baba ana nafsi. Mwana ana nyingine, tofauti, na nafsi kando.

Nikatazama hata viti vya enzi vikawekwa, na mmoja aliye mzee wa siku ameketi; mavazi yake yalikuwa meupe kama theluji, na nywele za kichwa chake kama sufu safi; kiti chake cha enzi kilikuwa miali ya moto, na gurudumu zake moto. Danieli 7:9.

Nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu akamkaribia huyo mzee wa siku, wakamleta karibu naye. Fungu 13.

Hapa kuna nafsi mbili, tofauti na kando katika utu wao. Maandiko yako wazi katika hili kama yalivyo katika mada yoyote ya Ukweli wa Bibilia.

Kwa sababu watu wa mataifa waliamini katika miungu fulani ambayo ilikuwa na mwili mmoja wenye kichwa zaidi ya kimoja na kwa sababu Kanisa la Roma lilipokea wazo hilo la mataifa, mateso ya milele, kuabudu wafu, alama ya msalaba, na pia Utatu, moja kwa moja kutoka kwa mataifa, fundisho la Utatu ni takatifu kuliko mateso ya milele, Sabbato ya Jumapili, pagatori, au fundisho lingine lolote la Kipagani la papa? HAPANA BILA SHAKA! Na ukweli kwamba Kristo sio mpatanishi katika Kanisa la Roma inaonyesha kwamba Utatu huharibu ukweli kwamba Kristo ni yeye, mpatanishi pekee.

Liitwalo Kanisa la Kikristo, Upapa, lilianzisha fundisho la Utatu, halimtambui kama mpatanishi pekee lakini wanaweka roho nyingi za wake kwa waume waliokufa kama wapatanishi. Ukishikilia fundisho la Utatu, kihalisia, Kristo sio mpatanishi wako tena...

Fundisho lote la Utatu ni la kigeni kabisa kwa mafundisho yote ya Bibilia na Roho ya Unabii. Ufunuo hautoi hata dokezo ndogo kulihusu. Wazo hili la kuchusha mno la mataifa halina nafasi katika ulimwengu wote huru wa Baba yetu Mtakatifu wa Mbinguni na Mwanawe, Bwana wetu na Mkombozi, Yesu Kristo....

Waadventista wa Sabbato wanadai kuchukua neno la Mungu kama mtawala mkuu na "Kutoka katika Babeli," na kukataa milele mizizi ya tamaduni ya Roma. Tukirejea kwa kutokufa kwa mioyo, pagatori, mateso ya milele na Sabbato ya Jumapili, hilo litakuwa chochote kuliko uasi (apostasy)? **Kama, hata hivyo, tunachechemea katika haya madogo, mafundisho makuu na kukubali na kufundisha mizizi hasa, fundisho la Kirumi, Utatu, na kufundisha kwamba Mwana wa Mungu hakufa, hata hivyo maneno yetu yanaonekana kuwa ya kiroho, hili ni lingini tofauti au lolote ndogo kuliko uasi? na Omega hasa wa uasi**?..." [From J. S .Washburn`s Letter in 1939.]

## Charles S. Longacre

(1871-1958)

*Kutoka kwa muswada wake katika mwaka wa 1946*

"Mimi ni Alfa na Omega, asema Bwana Mungu, Aliyeko, aliyekuwako na atakayekuja, Mwenyezi, Ufu. 1:8, Tena Bwana alisema: "Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho:" Ufu. 1:11.

**Sio kila kitu kina mwanzo wala kila kitu kina na mwisho. Mungu mwenyewe hakuwa na mwanzo na hatakuwa na mwisho. Yeye ni mwenye uwepo wake mwenyewe, ambaye hakuwa na mwanzo**. Umilele wenyewe haukuwa na mwanzo na wala hautakuwa na mwisho. Anga haina mwanzo na wala mwisho. Kila kitu kingine kilikuwa na mwanzo na kitakuwa na mwisho.

**Kuhusu Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, inasemwa katika Maandiko, "ni Mzaliwa wa pekee wa Baba." Mwana wa Mungu hakuumbwa kama viumbe wengine wanavyo fanywa kuweko. Sio wakuumbwa bali kiumbe wa kuzaliwa, akifurahia sifa zote za Baba yake. Kristo mwenyewe anaelezea uhusiano wake binafsi kwa Baba kama ifuatavyo: "Kama vile Baba alivyo na uzima ndani Yake, usiowa kukopa, kutolewa popote, asilia, huru, na wa kudumu milele, "vivyo hivyo amempa Mwana kuwa na uzima ndani Yake." Yohana 5:26**. Mungu alimpa Kristo "mamlaka ya kuhukumu pia kwa kuwa Yeye ni Mwana wa Adamu." Yohana 5:27. **Kama angekuwa Mungu kwa haki yake mwenyewe, Baba hangempa Kristo mamlaka katika kutoa hukumu lakini alipewa** "Kwa kuwa yeye ni Mwana wa Adamu." "Mimi siwezi kufanya jambo lo lote peke Yangu." Yohana 5:30.

Kama Kristo alikuwa Mungu kwa haki yake mwenyewe, wa milele pamoja na Baba, sawa na Baba, au mwenye uwepo wake mwenyewe, badala ya kuwa Amezaliwa na Baba, mbona Kristo alisema, "Mimi siwezi kufanya jambo lo lote peke Yangu... sitafuti kufanya mapenzi Yangu mwenyewe bali mapenzi ya Baba?" mbona Kristo akasema kujihusu, "kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwapo mwingine. Mimi, naam, mimi, ni Bwana, zaidi yangu mimi hapana mwokozi."? Isa. 43:10, 11.

Neno "Mungu" linaandikwa kwa herufi "M" kubwa, na katika kauli ambayo inafuata (fungu 12) Mungu alisema "hakukuwa mungu wageni miongoni mwenu." Hapa Bibilia inatumia herufi "m" ndoga ya mungu. **Fungu hili katika Isaya 43:10 linadhibitisha wazi kwamba, Kristo, Mkombozi pekee wa ulimwengu, alikuwa Mungu pekee ambaye aliumbwa. Kabla yangu "hakuumbwa Mungu awaye yote." Hivyo lazima tuhitimishe kwamba alikuwa wa kwanza na Mungu pekee ambaye aliumbwa, kwa**

**maana kabla ya yeye hakuumbwa Mungu awaye yote**.

**Kama kuna ukweli mmoja ambao Bibilia hufundisha, ni kwamba kuna Mungu mmoja tu na hakuna mwingine zaidi yake ambaye ni Mungu mkuu. Katika sura ya 15 ya Wakorintho wa pili, Paulo anafunza fundisho hili hivyo hakuwezi kuwa na shaka kwa utiifu na unyenyekevu wa Kristo kwa Baba. Paulo anasema: "Ndipo mwisho utafika, wakati atakapomkabidhi Mungu Baba Ufalme, akiisha angamiza kila utawala na kila mamlaka na nguvu. Kwa maana lazima Kristo atawale mpaka awe amewaweka adui zake wote chini ya miguu yake. Adui wa mwisho atakayeangamizwa ni mauti. Kwa maana Mungu ameweka vitu vyote chini ya miguu yake. Lakini isemapo kwamba, "Vitu vyote vimewekwa chini Yake, ni wazi kwamba Mungu aliyetiisha vitu vyote chini ya Kristo hayumo miongoni mwa hivyo vilivyotiishwa. Atakapokuwa amekwisha kutiisha vitu vyote chini ya Mwana, ndipo Mwana mwenyewe atatiishwa chini yake Yeye aliyetiisha vitu vyote, ili Mungu awe yote katika yote.**" 1 Kor. 15:24-28.

**Hapa Paulo anafundisha wazi kwamba Mungu hajinyenyekeshe kwa Kristo, bali Kristo anajinyenyekesha kwa Baba, aliye mpa mamlaka yote. Chochote Kristo alicho, mamlaka yoyote aliyonayo, sifa zote anazomiliki, zinaweza kuwa yote katika yote. Paulo anasema, "na ninyi ni wa Kristo, naye Kristo ni wa Mungu." 1 Kor. 3:23. Tena Paulo anasema: "Lakini napenda mfahamu kwamba kichwa cha kila mwanaume ni Kristo … nacho kichwa cha Kristo ni Mungu: "Nakwenda kwa Baba, kwani Baba ni mkuu kuliko Mimi.**" Yohana 14:28.

Lakini Paulo alifundisha kwamba Kristo alikuwa "sawa na Mungu," na kwamba Mungu mwenyewe "alimwinua" katika nafasi hiyo. Kwa kuwa Paulo anasema, "Kristo Yesu, Yeye ingawa alikuwa sawa na Mungu, hakuona kule kuwa sawa na Mungu ni kitu cha kushikamana nacho, bali alijifanya si kitu, akajifanya sawa na mtumwa, akazaliwa katika umbo la mwanadamu. Naye akiwa na umbo la mwanadamu, alijinyenyekeza hata mauti, naam, mauti ya msalaba! Kwa hiyo, Mungu alimtukuza sana na kumpa Jina lililo kuu kuliko kila jina, ili kwa Jina la Yesu, kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, vya duniani na vya chini ya nchi na kila ulimi ukiri ya kwamba Yesu Kristo ni Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba." Flp 2:5-11.

**Mbona tutoe utukufu kwa kutukuzwa kwa Kristo kuliko kila jina badala ya jina la Mungu mwenyewe, kwa Mungu Baba badala ya Kristo katika haki yake mwenyewe? Kwa sababu ni Mungu Baba ambaye amemtukuza.** Paulo anafanya ukweli huu mkuu wa Kristo kumtegemea Baba yake bado dhahiri zaidi anaposema kwa Timotheo: **"Nakuagiza mbele za Mungu avipaye vitu vyote uhai na mbele za Kristo Yesu ambaye alipokuwa anashuhudia mbele ya Pontio Pilato alikiri ukiri mzuri, uishike amri hii bila dosari wala lawama mpaka kuja kwake Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye Mungu atamleta kwa wakati wake mwenyewe, Yeye ahimidiwaye, aliye peke yake Mtawala, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. Yeye peke yake hapatikani na mauti, ambaye anakaa katika nuru isiyoweza kukaribiwa, ambaye hakuna mwanadamu aliyemwona wala awezaye kumwona. Heshima na uweza una Yeye milele.**" 1 Tim. 6:13-16.

**Mungu "peke yake hapatikani na mauti." Yeye pekee ndiye mwenye uwepo wake mwenyewe. Lakini alimpa Mwanawe alipozaliwa uzima sawa aliokuwa nao ndani yake, kwa hivyo Kristo alipoutoa uzima wake kama fidia kwa dhambi za ulimwengu, Yeye na Yeye pekee angefanya upatanisho kwa dhambi zote za ulimwengu, kwa sababu alifanya "dhabihu isiyokuwa na mwisho,"** na ilihitaji Dhabihi kama hiyo" kupatanisha kwa dhambi zote za wanadamu na malaika ambao walikuwa wametenda dhambi, ili kutosheleza mahitaji ya sheria ya Mungu na haki isiyokuwa na mwisho.

Tunaambiwa kwamba Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kwamba malaika hawangefanya upatanisho kwa dhambi zetu. Malaika walikuwa viumbe wenye dhambi kama tu wanadamu walivyo, lakini wanadamu ni viumbe wenye cheo cha chini. **Kristo alikuwa na umilele usiokuwa na masharti ukiwekwa juu yake wakati alizaliwa na Baba. Malaika walikuwa na umilele wa masharti ukiwekwa juu yao walipoumbwa na Kristo hapo mwanzo. Malaika ni wa milele lakini umilele wao ni wa masharti**. Kwa hivyo malaika hawafi lakini wanaendelea kuishi baada ya dhambi kama Shetani au Lusifa anavyoishi katika dhambi. Lakini kwa vile Lusifa na malaika walioasi wanafurahia umilele wa masharti, Mungu hatimaye atawaangamiza na kuchukua zawadi ya umilele ambao Kristo

aliweka kwao alipowaumba. Chochote ambacho Mungu huwekeza anaweza chukua wakati wowote anapoona vyema. Katika ufufuo, umilele utawekwa kwa kila mtakatifu ambaye atafufuliwa kwa uzima kupitia kwa Yesu Kristo. Kisha na sio hadi wakati huo ndio uzima wa milele utawekwa kwa Wakristo. "**Huu ndio ushuhuda kwamba, Mungu ametupa uzima wa milele, nao huo uzima umo katika Mwanawe." 1 Yohana 5:11. Lakini pia uzima huu wa milele pia uko katika Baba. Kwa kuwa Yohana: "Uzima huo ulidhihirishwa … uzima wa milele … ni pamoja Baba." 1 Yohana 1:2, 3. Hapa tunaambiwa wazi kwamba uzima wa milele sawa, kudumu milele ambako kuna Baba, kulidhihirishwa katika Mwanawe, na kutarejeshwa katika ufufuo na utapewa watakatifu wote katika Kristo. Lakini tusisahau ni umilele wa kupewa. Kwa hivyo tunaona kwamba uzima wa milele na kutokufa kutarejeshwa kwa viumbe ambao hawakuwepo awali na Mungu**. Ni uzima wa milele sawa ulio na Mungu, na wakati ambao wanadamu watafanywa kutokufa unasemwa kwamba "wakijawa na utimilifu wote wa Uungu." Efe. 3:19.

**Lakini Kristo, Mwana wa pekee wa Baba, alifanywa "mung'ao halisi" wa nafsi ya Baba. Mungu hakumfanya tu kuwa Mkombozi wa wanadamu, bali alimfanya "mrithi wa vitu vyote," "ambaye amemweka kuwa mrithi wa vitu vyote, alifanyika bora kuliko malaika kama Jina alilorithi lilivyo bora kuliko lao. Kwa maana ni malaika yupi ambaye wakati wo wote Mungu alipata kumwambia, "Wewe ni Mwanangu, leo Mimi nimekuzaa?" Ebr. 1:2-5. Hapa tunaambiwa kwamba kauli "Wewe ni Mwanangu, leo Mimi nimekuzaa," inarejelea Kristo tu na wala sio malaika yeyote. Basi lazima kuwe na wakati, siku, ambayo Mwana wa Mungu alizaliwa na Baba. Katika siku hiyo, Baba alisema kwa Mwana wa pekee: "Kiti chako cha enzi, Ee Mungu, kitadumu milele na milele… kwa hiyo Mungu, Mungu wako, amekuweka juu ya wenzako kwa kukupaka mafuta ya furaha. Hapo mwanzo, Ee Bwana, uliweka misingi ya dunia, nazo mbingu ni kazi ya mikono Yako.**" Ebr. 1:8-10. Paulo anasema: "Nazidi kumwomba Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa utukufu, awajalieni ninyi roho ya hekima na ya ufunuo, ili mpate kumjua zaidi." Efe. 1:17. **Baba ni Mungu wa Bwana Yesu Kristo – ni Baba na Kristo ni Mwanawe mzaliwa wa pekee.**

Tena Paulo anasema. "Kuna mwili mmoja na Roho mmoja … Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja, Mungu mmoja ambaye ni Baba wa wote, aliye juu ya yote, katika yote na ndani ya yote." Efe. 4:4-6. Tena Paulo anasema: "Lakini kwetu sisi yuko Mungu mmoja, aliye Baba, ambaye vitu vyote vyatoka Kwake na kwa ajili Yake sisi twaishi na kuna Bwana mmoja tu, Yesu Kristo, ambaye kwa Yeye vitu vyote vimekuwepo na kwa Yeye sisi tunaishi …**kuna Mungu mmoja tu." 1 Kor. 8:6, 4. Nabii Malaki anasema: "Je! Sisi sote hatuna Baba mmoja? Mungu aliyetuumba siye mmoja tu?"** Mal. 2:10.

Katika kitabu "Patriarchs and Prophets,"**Dada White ananukuu Methali. 8:22-26, na anatumia mafungu hayo kwa uwepo wa Kristo awali.** Fungu asilia na Kiebrania linasema: "Bwana alikuwa nami - mwanzo wa njia yake, Kabla ya matendo yake ya kale. Nalitukuka tokea milele... Alipoiagiza misingi ya nchi; Ndipo nilipokuwa pamoja naye, kama stadi wa kazi; Nikawa furaha yake kila siku; Nikifurahi daima mbele zake." **Katika Kiebrania asili, re'shiyth (raysheeth), ambalo linamaanisha "mwanzo," ni neno sawa hasa kama tunavyopata katika Mwanz. 1:1. Lakini katika Mwanz. 1:1 neno (raysheeth) lina kihusishi "hapo" kikitangulia neno la Kiebrania "bere-shiyth." Kihusishi hicho (hapo) hakihusiani na neno (ray-sheeth) katika Methali. 8:22. Ikitafsiriwa kwa kawaida, inafaa kusoma "Bwana alikuwa nami - mwanzo wa njia yake." Pili kauli inatumika katika Methali. 8:22-30. Kabla "haijaweko dunia… nalizaliwa.**" **Neno nalizaliwa linatoka katika neno moja la Kiebrania, Chiyl (Kheel) ambalo kwa kawaida linamaanisha, kuzaliwa, kutolewa au kutengenezwa**. Hapa Kristo akizungumza kujihusu alisema: "Nalizaliwa, Wakati zisipokuwako chemchemi zilizojaa maji ... au Kabla haijawako dunia."

**Nalizaliwa, naliumbwa. Kauli hizi zinakubaliana na kile ambacho Kristo alisema kujihusu katika Isaya 43:10,11: "mpate kujua, na kuniamini, na kufahamu ya kuwa mimi ndiye; kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwapo mwingine. Mimi, naam, mimi, ni Bwana, zaidi yangu mimi hapana mwokozi**." Tafsiri nyingine ya fungu hili inasoma: "kabla yangu hakuna chochote kiliumbwa cha Mungu." mdokezo katika tafsiri yetu ya King James ni kwamba Yeye, Kristo, "aliumbwa" kama Mungu, sawa na Mungu, lakini zaidi yake hakuna Mungu

aliyeumbwa na zaidi yake hapana mkombozi aliyeteuliwa. Lakini tafsiri hiyo nyingine ambayo imenukuliwa humfanya Mwana wa Mungu "mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote," kama Paulo anavyoiweka katika Kol. 1:15. Kristo mwenyewe anakubali kwamba mambo ya siri ni ya Mungu, na kwamba yeye mwenyewe kama Mwana wa Mungu, hajui siku wala saa ya marejeo yake ya pili katika dunia hii. Yesu alisema: **"Lakini kwa habari ya siku ile na saa hakuna ye yote ajuaye, hata malaika walioko mbinguni wala hata Mwana hajui, ila Baba peke Yake." Marko 13:32. Na katika Matt. 24:36, Yesu anasema, "ila Baba peke yake" anajua siku hiyo na saa. Kristo anatambua kwamba chote alichokuwa nacho hekima, uwezo, mamlaka, na uzima wenyewe, vyote alikuwa amepewa kutoka kwa Baba. Kutukuka kwake kulitoka kwa Baba.**

## WAANZILISHI WENGINE

### C. W. Stone

"Neno basi ni Kristo. **Fungu linazungumza kuhusu asili yake.** Ni mzaliwa wa pekee wa *Baba*. Jinsi tu alikuja kuwepo Bibilia *haitwambii* zaidi dhahiri; lakini kwa kauli hii na zingine kama hizi katika Maandiko tunaweza amini kwamba Kristo alikuja kuwepo kwa njia tofauti na ile viumbe wengine walikuja kuwepo mwanzo; **kwamba alitoka katika nafsi ya Baba akiwa kwa njia ambayo sio muhimu kwetu kufahamu.**"{C. W. Stone, *The* Captain o*f* our Salvation, p. 17. 1886}

### A. J. Dennis

**"Ni utata upi unapatikana kwa istilahi zinazopatikana katika imani ya Utatu**: "katika umoja wa kichwa hiki kuna watu watatu, wa kiini sawa, uwezo, na umilele, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Kuna mambo mengi ambayo ni ya ajabu, yameandikwa katika neno la Mungu, **lakini tunaweza chukulia bila hofu kwamba Mungu kamwe hatuiti kuamini yasiyowezekana. Lakini imani (Creeds) mara nyingi hufanya hivyo**." {A. J. Dennis, Signs of the Times, May 22, 1879}

## A. J. Morton

"Roho mtakatifu ana uungu kwa sababu hutoka katika uungu. Kamwe hauwezi tenganisha uungu kutoka kwa Roho wa Mungu na Kristo kama unavyoweza tenganisha uungu kutoka kwa Mungu na Kristo. Kwa hivyo, ni, uwepo wa Roho katika ahadi za Mungu ndio hutuwezesha asili takatifu kutoka kwa ahadi hizo." {A. J. Morton, Signs of the Times, October 26, 1891, p. 342}

## D. W. Hull

"Msimamo wa kuyumba unaoshikiliwa na wengi kuhusiana na Utatu, kama unavyoitwa, bila shaka, umekuwa chanzo cha makosa mengine. Mitazamo potofu ya uungu wa Kristo inaweza tuongoza katika kosa kuhusiana na hali ya upatanisho. … Fundisho ambalo tunapendekeza kuchunguza lilianzishwa na Baraza la Nice*, A. D., 325,* **na tangu kipindi hicho, watu ambao hawaamini lengo hili teule, wameshutumiwa na papa na askofu, kama wazushi hatari**. Ni kwa sababu ya kutoamini fundisho hili, Uariani walitangazwa kuwa waovu katika A. D., 513. **Kama tunavyoweza pata fundisho hili sio mbali na asili ya "Mtu wa Dhambi," na tunapopata findisho hili katika wakati huo ambao lilianzishwa kwa nguvu kuliko kwa njia nyingine, tunadai haki ya kuchunguza suala hili, na kuthibitisha gololi ya Maandiko kuhusiana na mada hii.** Hapa tu nitakutana na swali ambalo linaulizwa sana, ambalo ni, unaamini katika Uungu wa Kristo? Bila shaka tunaamini; lakini hatuami, kama Somo la kanisa la M. E. linavyofundisha, kwamba Kristo ndiye Mungu wa milele; kwamba sehemu ya ubinadamu ilikuwa Mwana, na sehemu ya uungu ilikuwa Baba." {D. W. Hull, Review *&* Herald, November 10, 1859}

## J. M. Stephenson

Stephenson alikuwa mwongofu wa J. H. Waggoner. Wakati wa ugeni wa ulinganishi kwa kifupi miongoni mwa Waadventista wa Sabbato, Stephenson aliandika makala mengi katika Tathmini akiweka katika uwazi msimamo wa kanisa kuhusu Uungu. Wakati alishindwa, aliiacha imani yake ya awali, na akaikataa Sabbato na ukweli mwingine ambao alikuwa amesoma kwa umoja na ndugu.

**“**Kwa kurejelea heshima yake, alifanyika Mwana wa Mungu, **kabla ya mwili wake**. Sikia lugha yake mwenyewe: [Yohana 7:18; 10:36; 1 Yohana 4:9, 10 imenukuliwa] wazo la kutumwa linaashiria kwamba alikuwa Mwana wa Mungu ili atumwe. Kudhani vingine ni kudhani kwamba Baba anaweza mtuma mwanawe mishene kabla mwana huyo hajakuwepo, jambo ambalo linaweza dhihirishwa kuwa halina mantiki. “Kusema kwamba Mungu alimtuma Mwanawe kwa mfano wa mwili wa dhambi,” ni sawa na kusema kwamba Mwana wa Mungu alichukua asili yetu; kwa hivyo lazima alikuwa Mwana wa Mungu kabla ya kufanyika mwili.**”** {J. M. Stephenson, Review & Herald, November 7, 1854}

**“Kuwa Mwana wa pekee wa Mungu lazima ifahamike kwa maana tofauti kuliko kuwa Mwana kwa uumbaji;** kwa kuwa kwa namna hiyo viumbe vyote vimefanywa wanawe. Wala haiwezi rejelea kuzaliwa kwake kwa muujiza, na bikira Maria, kwa Roho Mtakatifu; kwa sababu anawasilishwa kwa jina hili kuu zaidi ya miaka elfu nne kabla ya kushuka kwake katika kijiji cha Bethlehemu. Zaidi ya hilo, anawasilishwa akitukuzwa juu kuliko vyeo vya juu vya wanadamu na malaika katika asili yake asilia. Kwa hivyo lazima afahamike kuwa Mwana wa Mungu na kwa namna ya juu zaidi kuliko kiumbe awaye yote. **kuwa kwake mzaliwa wa pekee wa Baba kunamaanisha kwamba hakuna mwingine ila yeye alizaliwa hivyo; kwa hivyo, yeye ni, kwa kweli na uhalisia mzaliwa wa Pekee wa Mungu; na kwa hivyo lazima awe na Uungu; yaani, kuwa mshirika asili wa Uungu**. … **Dhana ya Baba na Mwana inapendekeza kipaumbele cha uwepo wa mmoja, na uwepo wa mwingine baadaye. Kusema kwamba Mwana ana umri sawa na Baba yake, ni ukinzani halali wa istilahi. Ni jambo ambalo kiasilia haliwezekani, Baba kuwa mchanga kama Mwanawe, au Mwana kuwa mkongwe kama Baba.** Kama itasemwa kwamba istilahi hii imetumika katika njia ambayo imeshughulikiwa, bado inasalia kuelezewa, mbona Baba atumie jina kuu lenye mshikamano, na la kupendeza zaidi kuonyesha uhusiano wake mwenyewe na Bwana wetu, jina ambalo, katika maana yake yenye mshikamano, linaweza kinzana na wazo ambalo alitaka kupitisha**.**

**Kama waandishi walioongozwa na Roho walitaka kupitisha dhana ya uwepo sawa, na umilele wa Baba na Mwana, hawangetumia istilahi**

**ambazo haziendani kabisa**. Na hili, Wana-utatu, wamekuwa werevu. Bw. Fuller, ingawaje Mwana-utatu, kwa uaminifu alithamini, katika hitimisho ya kazi yake juu ya Uwana wa Kristo, kwamba, "katika mpangilio wa maumbile, Baba lazima alikuwepo **Kabla ya** Mwana." … Hili linampa "mzaliwa wa pekee wa Baba" (tazama [Yohana 1] fungu 14) uwepo wa akili kabla ya tendo la kwanza la uwezo wa uumbaji kufanyika, na inathibitisha kwamba ni asili yake ya Uungu inayozungumziwa hapa; na hiyo pia, kwa uhusiano na uumbaji wa vitu vyote. Katika fungu la 14, Neno huyu, ambaye alikuwako "hapo mwanzo" "pamoja na Mungu," na ambaye kwake "vitu vyote viliumbwa, ambavyo vilifanyika," anatangazwa kuwa "Mwana wa pekee wa Mungu," **hivyo kufundisha kwamba katika umbile lake kuu alikuwa mzaliwa wa pekee; na kwa sababu hiyo, lazima alikuwa na mwanzo**.**"** {J. M. Stephenson, Review & Herald, November 14, 1854}

# Wacha Waanzilishi Watambue Ukweli

Wakati nguvu za Mungu zinashuhudia ukweli ni nini, kwamba ukweli utasimama milele kama ukweli. Hakuna dhana ya baadaye, kinyume cha nuru ambayo Mungu ametoa inapaswa kukubaliwa. Watu watazuka na tafsiri ya maandiko ambayo ni ukweli kwao, lakini ambayo sio ukweli. Ukweli wa wakati huu, Mungu ametupa kama msingi wa imani yetu. Yeye mwenyewe ametufundisha ukweli ni nini. Mmoja atainuka, na mwingine pia, na nuru ambayo ni kinyume na nuru ambayo Mungu ametupa chini ya onyesho la Roho Mtakatifu.

Wachache bado wako hai ambao walipitia uzoefu uliopatikana katika kuanzisha ukweli huu. Mungu kwa neema amehifadhi maisha yao yajirudierudie hadi kufungwa kwa maisha yao, uzoefu waliopitia hata kama Yohana alipitia hadi mwisho wa maisha yake. Na wabeba-kiwangogezi ambao wameanguka katika kifo, watazungumza kupitia kwa kuchapishwa upya kwa hati zao. Ninaelekezwa kwamba kwa hivyo sauti zao zitasikika. Watabeba ushahidi wao wa kile kilicho ukweli wa wakati wa sasa. {Ellen White, Counsels to Writers and Editors – uk. 31, Par.2, p. 32, Par.1}

**maranathamedia.com**